# Nipashe

Alhamisi Agosti 13, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580309

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11



## Mwanafunzi darasa la tano adaiwa kubakwa kwenye mkesha wa harusi

UKURASA 3

# Vyama vya siasa vyamjibu Sirro



UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

### RUHINDA: MKAPA ALILENGA KUJENGA UJAMAA KATIKA MAZINGIRA MAPYA

SEHEMU ya tatu na ya mwisho ya ushuhuda wa Mzee Ferdinand Ruhinda juu ya rafiki yake wa zaidi ya miaka 50, Benjamin Mkapa, Rais wa tatu wa Tanzania, aliyefariki dunia Julai 23 na kuzikwa Julai 29, mwaka huu, kijijini kwao, Lupaso, Mtwara. Endelea kusoma...

## Tundu Lissu sasa asaka wadhamini Kaskazini

UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikata utepe kufungua Jengo la Intelijensia la Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Makao Makuu jijini Dodoma, jana. Kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi wa Umma na Utawala Bora), George Mkuchika, (wa tatu kushoto) ni Naibu Waziri, Mary Mwanjelwa na (wa pili kulia) ni Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbung'o. **PICHA: OWM**





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store




## Wavuvi wamlalamikia Waziri sheria, kanuni

UKURASA 2


**MICHEZO** MO MO MO MORRISOOOOON! UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Kamishna wa Polisi (Operesheni na Mafunzo), Liberatus Sabas, akizungumza na askari wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) Mkoa wa Morogoro jana, alipokuwa akikagua utayari wa askari hao, katika kukabiliana na vitendo vya kihalifu kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu. **PICHA: FRANK KAUNDULA**

# Vyama vya siasa vyamjibu Sirro

**Na Salome Kitomari**

VYAMA vya siasa nchini vimeliomba Jeshi la Polisi kutenda haki na kutoonyesha kupendelea upande wowote kuelekea kwenye uchaguzi, ili kutunza amani na utulivu.

Kwa upande wake, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimempongeza Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, kwa kazi nzuri ya kulinda raia na mali zao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, viongozi hao walisema iwapo jeshi hilo litasimamia sheria, kanuni na taratibu bila ubaguzi au kubeba chama chochote cha siasa, hakutakuwa na uvunjifu wa amani utakaotokea.

Viongozi hao walikuwa wakizungumzia kauli ya IGP Simon Sirro, aliyoitoa mwanzoni mwa wiki akihojiwa na Kituo cha luninga cha ITV, ambaye aliwaonya wanasiasa wanaoanzisha shari kupitia matamshi yao.

Msemaji wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tumaini Makene, alisema CHADEMA inashangazwa namna ambavyo Polisi hawajachukua hatua kwa watu waliotoa kauli za vitisho dhidi ya mgombea urais wao, Tundu Lissu, ambazo zinaashiria shari na kutaka kuvuruga amani.

"Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, alishamwandikia barua IGP ili achukuliwe hatua dhidi ya waliotaka kumuua Lissu mwaka 2017 na wanaotoa lugha za kutishia uhai wake, hadi sasa hakuna majibu na badala yake kinachozungumzwa ni kitu kingine," alisema.

Alisema chama hicho kitafanya siasa kwa mujibu wa kanuni na sheria za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na kwamba kampeni zao zote zitazingatia hayo na si maelekezo ya polisi.

"Kama polisi wanataka uchaguzi uwe wa amani na utulivu watende haki, waachie wananchi wafanye uamuzi kwenye sanduku la kura, kusiwe na maelekezo ya mara kwa mara kwa vyama," alisema.

Makene alitolea mfano wa matukio ya hivi karibuni ya mgombea wa ubunge Jimbo la Ruangwa kusakwa na polisi, huku wanachama wao waliokuwa wanamsindikiza mgombea ubunge huko Mpwapwa kurejesha fomu kukamatwa.

"Jeshi la Polisi litende haki kwa vyama vyote, tunafahamu maadili na sheria na si kwa maelekezo ya jeshi la polisi," alibainisha.

**CCM YAMPONGEZA IGP**

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM anayeshughulikia Siasa na Uhusiano wa kimataifa, Kanali mstaafu, Ngemela Lubinga, alisema CCM kupitia Mwenyekiti wake, Rais John Magufuli, ndiyo walianza kuzungumza na kusisitiza amani na utulivu wakati wa uchaguzi.

"Sisi ndiyo tulianza Mwenyekiti wetu alishasema kampeni ziwe za amani na utulivu, vyombo vya ulinzi na usalama vilishaagizwa kuhakikisha amani na utulivu vinakuwapo wakati wote," alisema. "Tunamshukuru na kumpongeza IGP Sirro kwa kutimiza wajibu wake," alisema.

**ACT-WAZALENDO**

Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema vyama vinafanyakazi kwa mujibu wa Katiba na sheria, na kwamba polisi hawafanyi kazi kwa matakwa ya mtu au chama chochote.

"Hatuna shari, tunafuata sheria, uchaguzi ukifuata taratibu, mshindi akapewa ushindi wake tutamaliza kwa amani," alisema.

"Tukiona ushindi wetu unaporwa hapo ndiyo hatutakubali, tunachotaka haki itendeke na hiyo shari haitaonekana," alisema Shaibu.

Kwa mujibu wa Shaibu, Jeshi ni chombo kilichopo kisheria kulinda usalama wa raia na mali zao, na kwamba kazi yao si kupendelea chama chochote cha siasa.

"Wakifanya kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni hakuna vurugu itakayotokea, ila kuna ushahidi kuwa litakuwa chanzo," alisema.

**KAULI YA CUF**

Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi Taifa wa CUF, Juma Kilaghai, alisema ni vyema polisi wakatenda haki, huku akirejea moja ya video iliyosambaa ikimwonyesha mmoja wa makamanda wa polisi akiwa kwenye mkutano wa CCM akizungumza, lakini IGP Sirro hakutoa kauli yoyote.

CUF inaangalia na ikiona kiashiria chochote italijulisha Jeshi la Polisi, mfano sasa baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi hawajui kinachoendelea wakati baadhi ya wagombea wananyimwa kanuni na nyaraka muhimu.

"Haya yote amani inaweza kuvurugika, tukikutana na hali hiyo tunaiandikia Tume, tunataka haki itendeke kwa vyama vyote kusiwe na kubeba chama chochote," alisema.

**NCCR-MAGEUZI**

Mkuu wa Idara ya Uenezi na Mahusiano ya Umma, Edward Simbeye, alisema chama hicho hakitafanya siasa za kulichokoza Jeshi la Polisi bali zenye tija kwa wananchi zitakazostawisha amani, weledi na utulivu kwa maslahi ya nchi.

"Hatutakuwa sehemu ya kulichokoza Jeshi la Polisi na wao wasiwe chanzo cha kuvichokoza vyama vya siasa, litende haki," alisema.

# Wavuvi walia na kanuni za uvuvi

**Na Romana Mallya**

WAVUVI wa Soko la Samaki la Kimataifa Feri jijini Dar es Salaam, wamepinga kanuni za uvuvi ya mwaka 2020 wakidai siyo rafiki kwao na adhabu zake hazitekelezeki.

Waliwasilisha kilio chao hicho kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, baada ya kufanya ziara ya kushtukiza sokoni huko na kufanya kikao nao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti mbele ya waziri huyo, wavuvi hao walisema kanuni hizo siyo rafiki kwao na hazikuzingatia mapendekezo waliyoyatoa awali.

Mratibu wa Vyama vya Sekta ya Uvuvi Ukanda wa Pwani, Mohamed Muhidini, alimwambia waziri huyo kuwa, kanuni za mwaka 2020 siyo rafiki kwao, hivyo waliamua kusitisha shughuli za uvuvi baharini kwa muda.

"Kanuni zilizopo siyo rafiki kwetu, hukumu zake ni ngumu, hazitekelezeki na zina mengi ambayo mpaka unakuja hapa ni kwamba mmeshayapitia.

"Faini zilizopo siyo rafiki, maelekezo kuhusu matumizi ya zana za uvuvi yanakanganya, maeneo ya kazi tuliyoelekezwa na kanuni siyo rafiki, unapomwambia mtu avue mita 50 kwa ekolojia ya hapa ni bahari kuu ambapo vyombo vyetu havina uwezo huo," alilalamika.

Faki Faki, mmoja wa wavuvi hao alisema kuwa Oktoba walikutana Dodoma kwa ajili ya kutoa maoni yao ili kuboresha kanuni hizo, lakini hayakuzingatiwa.

"Tulichangia, tukazindua rasimu ya kanuni ukumbi wa Karimjee, tukatoa maoni, bahati nzuri Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mahmoad Mgimwa, alituambia 'ikiwa maoni yenu hayapo niambieni'.

"Nilikuuliza waziri umeleta hii rasimu isije ikawa umeshaipitia hii kusema toeni maoni ni kizungumkuti kumbe ndiyo jibu langu, hongera kwa hilo," alisema.

Akizungumzia kanuni hizo, Waziri Mpina alisema awali alitangaza kuwa atafumua Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009 kwa sababu teknolojia na mazingira ya uvuvi yamebadilika. Alisema aliona zifumuliwe ili kuweka mazingira bora kwa ajili ya wavuvi kwa sababu shabaha ya serikali siyo kuwakwaza wavuvi.

"Kulikuwa na mambo kama tozo zilikuwa kubwa, leseni nayo gharama zilikuwa kubwa, mwanzo kanuni ya tozo ya samaki mfano dagaa wa bahari ilikuwa kuwauza nje ya nchi ni dola moja na wa Ziwa Tanganyika dola 1.5.

"Nimepunguza kutoka dola moja hadi dola 0.3, mkasema hata hiyo hamtauza, imeshuka zaidi hadi dola 0.16, leseni ya kuuza mazao ya uvuvi, mvuvi wa dagaa anapotaka leseni ili kuyasafirisha kuuza nje ya nchi ilikuwa dola 1,000 na sasa ni dola 250, hili ni punguzo la asilimia 75," alibainisha.

Alisema mazao mengine kama kamba miti leseni ilikuwa dola 2,500 na sasa ni dola 500 wakati wafanyabiashara wa kaa ilikuwa dola 2,500 na kwa sasa ni dola 500.

Mpina pia alisema serikali imeamua kuanzia sasa leseni itakuwa ni moja na itatambulika kama leseni ya kuvua Bahari ya Hindi au ukanda wa Pwani kulingana na eneo.

"Ilikuwa ikifika Januari Mosi ulikuwa huruhusiwi kuingia majini mpaka ukate leseni, tumerekebisha hakuna mtu atakayemkamata mvuvi, mtakata polepole kwa miezi mitatu mpaka Machi," alisema.

Waziri huo alisema soko hilo kila mwezi linakusanya Sh. milioni 100 ambazo zilikuwa zikitumika kwa matumizi ya kawaida, lakini kwa sasa wanabakiza Sh. milioni 30 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu.

"Vyoo vilikuwa vilevile, vimejengwa, majengo yamejengwa, tulikuta watu wanaweka samaki kwenye mchanga na sasa yapo maeneo na ukarabati bado unaendelea," alisema.

HABARI KITAIFA

## Tundu Lissu kusaka wadhamini Kaskazini

**Na Woinde Shiza,** ARUSHA

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, na mgombea mwenza wake, Salim Mwalimu, wanatarajia kutua Arusha kesho kwa ajili ya kusaka wadhamini katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari kwenye ofisi za kanda za chama hicho.

Alisema wanatarajia kuwapokea Lissu na Mwalimu kwenye Uwanja wa Ndege wa Arusha na baadaye watakuwa na mikutano mifupi jijini.

Lema aliwataka wanachama wa CHADEMA kujitokeza kwa wingi kuwapokea wagombea wao hao kwa kuwa ngome kuu ya chama hicho ni Kanda ya Kaskazini.

“Baada ya kumpokea, tutakuja naye hapa, wanachama pamoja na viongozi wa chama waliojitokeza kumleta mpaka ofisini na kufanya mkutano mfupi kwa ajili ya kumdhamini na hotuba fupi itakuwapo.

“Likiisha hilo, mgombea wetu ataondoka na kuelekea katika maeneo mengine na kila eneo tayari ratiba zimeshatolewa na maelekezo ya kiofisi tayari, kinachotakiwa ni tujiandae tu kwa ugeni huo.

“Niwaombe tu wananchi wajitokeze kwa wingi kuja kumdhamini mgombea na safari hii sisi kama CHADEMA tumejipanga kupeleka zaidi ya idadi ya wadhamini ambao tume wamependekeza,” alisema Lema.

Kiongozi huyo wa kanda pia alisema uchukuaji wa fomu za kuomba kuwania nafasi za ubunge na udiwani ulianza jana na baadhi ya wanachama wameshachukua.

Lema alisema kuwa yeye hatachukua fomu wiki hii na atangaza rasmi siku ambayo atachukua fomu ya kuomba kuteuliwa kuwania tena ubunge wa Arusha Mjini.

“Tunaendelea kuangalia jinsi uchukuaji wa fomu unavyoenda na tuna watu kila upande wanafuatilia suala hili. Tunafuatilia kila mahali na niseme tu kwamba hatutakubali matendo maovu yaliyofanywa kipindi cha uchaguzi wa serikali za mitaa yajirudie kipindi hiki,” alisema.

Lema alitamba kuwa CHADEMA imetoa elimu kwa wagombea wake kufanya siasa za amani huku akiahidi kuwa hawatafanya fujo yoyote na watafuata sheria zote za uchaguzi zilizoelekezwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

# Mwanafunzi la tano adaiwa kubakwa mkesha wa harusi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MWANAFUNZI wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Kilago Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga(jina tunalihifadhi), amedaiwa kubakwa usiku wa mkesha wa sherehe ya harusi.

Kwa mujibu wa kaka wa mwanafunzi huyo, Phabian Manyanda, tukio hilo lilitokea siku Julai 31, mwaka huu majira ya saa tatu usiku wakati wa mkesha wa sherehe ya harusi iliyokuwa ikifanyika kijiji kwao jirani na makazi yao.

Alisema kuwa siku hiyo walifika nyumbani mabinti wawili ambao ni majirani akiwataja kwa majina ya Zawadi na Nyamizi ambao waliondoka na mdogo wake kwenda kwenye sherehe hiyo na baadaye walimrejesha nyumbani majira ya saa saba usiku akiwa ana hali mbaya kiaya.

Manyanda alidai kuwa, siku iliyofuata hali ya mdogo wake ilizidi kuwa mbaya na walimpeleka zahanati ya Kata ya Kilago na alipopimwa, daktari alisema alikuwa na maambukizo makali kwenye njia ya mkojo (UTI) na alipatiwa dawa.

Hata hivyo, Manyanda alisema kuwa licha ya matibabu hayo, Agosti 2 mwaka huu, walimpeleka tena kwenye zahanati ya mtu binafsi iliyoko kijijini huko na baada ya vipimo, ilibainika ana maambukizi ya malaria, jambo ambalo liliwatia hofu na kuhisi kuna jambo ambalo linaendelea kwa ndugu yao huyo. Manyanda alisema kuwa kutokana na hofu hiyo, siku iliyofuata walichukua uamuzi wa kumpeleka katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama kwa ajili ya vipimo zaidi, lakini mdogo wake alisita kuongea na madaktari na walipozungumza naye kwa ‘lugha laini’, aliwaambia ukweli kuwa alibakwa na mtu asiyemfahamu.

“Daktari aliyetupokea na kutupatia huduma alichukua uamuzi wa kuzungumza naye kirafiki na kuelezwa kuwa alichukuliwa na marafiki zake, Zawadi na Nyamizi wakidai wanakwenda kununua soda, waliofika eneo la jengo ambalo halijakamilika, alivutwa na mtu asiyemjua na kumwingilia,” alidai Manyanda.

Aliendelea kueleza kuwa baada ya kubakwa, aliyetenda kitendo hicho alikimbia huku mabinti waliompeleka kwa mtu huyo wakimtisha kuwa akimwambia mtu yeyote, atakufa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Debora Magiligimba, alikiri kuwa na taarifa za tukio hilo na kubainisha kuwa upelezi wa kumbaini aliyetenda kitendo hicho unaendelea ili afikishwe mahakamani.



# Majaliwa aipa TAKUKURU maagizo mazito

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuhakikisha Watanzania hawarubuniwi ili watumie vizuri utashi wao wa kisiasa kuchagua viongozi bora.

Alitoa agizo hilo jana alipofungua jengo la Intelijensia TAKUKURU Makao Makuu, Dodoma na kuwasihi watumie vizuri ofisi hiyo kukusanya taarifa muhimu za kiintelijensia zinazowahusu wagombea, vyama au wananchi watakaojihusisha na rushwa kwenye uchaguzi mkuu.

"Sote tunatambua kuwa Oktoba, mwaka huu, taifa letu litaendesha uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, hivyo mna jukumu zito la kuhakikisha Watanzania hawarubuniwi na msimwonee au kumpendelea yeyote kwa maslahi yenu binafsi," alisema.

Waziri Mkuu alisema wananchi wanatakiwa kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura Oktoba 28 na kwamba wana wajibu wa kuchagua serikali bora na kiongozi bora atakayewaletea maendeleo.

"Chagueni kiongozi mwenye maono, aliyetenda na atakayetenda. Tayari tumeshuhudia mking'ata baadhi ya wagombea waliojihusisha na vitendo vya rushwa kwenye hatua za awali za uteuzi wa wagombea kupitia vyama vyao. Msiache, endeleeni kukaza uzi na kuwadhibiti wote wenye kujihusisha na vitendo hivyo," alisisitiza.

"Niungane pia na Mhesimiwa Rais John Magufuli kuwasihi wanasiasa na wagombea wenzangu wa nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi mkuu Oktoba, tuache kutumia rushwa kwa lengo la kununua uongozi," aliongeza.

Alisema kuelekea uchaguzi mkuu ni vyema Watanzania na viongozi wakazingatia nasaha za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, katika moja ya hotuba zake alipowataka wajiulize kwamba mgombea anayetumia rushwa kununua kura amepata wapi fedha hizo na je, akipata uongozi, fedha hizo atazirudishaje?

"Kwa hivyo, nasi ifike mahala tuwahoji hawa wanaotutia doa. Je, wewe mwenzetu unayetumia rushwa kununua uongozi umepata wapi fedha hizo? Na je, tukikuchagua, utarejesha vipi fedha hizo? Nitoe wito kwa Watanzania wote, msikubali kuwachagua wagombea wanaotumia rushwa ili kupata nafasi za uongozi," alisema.

Waziri Mkuu ametumia fursa hiyo kuwapongeza viongozi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na watendaji wa TAKUKURU kwa kusimamia vyema mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi ndani na nje ya serikali.

Alisema hatua hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa kudhibiti wa matumizi ya ovyo ya fedha za umma, kuongeza usimamizi katika ukusanyaji wa mapato ya serikali na kuziba mianya ya ukwepaji kodi.

Pia alisema ni lazima wafanye uchunguzi wa kutosha juu ya matumizi ya fedha zote za umma na kujua kama matumizi hayo yanaenda sambamba na matakwa ya kisheria na pale ambapo watabaini ukiukwaji wa sheria wachukue hatua.

"Nyote mtakubaliana nami kuwa miongoni mwa mambo yaliyopewa uzito mkubwa na serikali ya awamu ya tano ni kuimarisha na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi.

"Rais Magufuli amemudu kurejesha imani ya Watanzania kwa watumishi wa umma na zaidi ya yote amerejesha uwajibikaji. Ni ukweli usiopingika kwamba tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa kulikabili tatizo la rushwa na ufisadi ndani ya taifa letu," alisema.

Ufunguzi huo ulihudhuliwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kapteni Mstaafu George Mkuchika; na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo.

Wengine Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mary Mwanjelwa, Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Charles Kicheere, Katibu Mkuu Ikulu, Dk. Moses Kusiluka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dk. Binilith Mahenge na maofisa wengine wa serikali.




Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Rose Reuben, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaaam jana, wakati akitoa tamko la pamoja na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF), na Global Peace Foundation (GPF), kuhusu mapendekezo yao kwa vyama vya siasa na wadau wingine wa uchanguzi, kuondoa changamoto zote zilizochangia ushiriki duni wa wanawake katika siasa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mchungaji kortini madai kubaka mwanafunzi

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MCHUNGAJI wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Chalinze, ambaye pia ni Mkuu wa Jimbo la Chalinze, Boniface Mgalula, amefikishwa katika Mahakama ya Mwanzo Lugoba mkoani Pwani akituhumiwa kumbaka mwanafunzi na kumpa mimba.

Akisoma mashtaka mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Bagamoyo, Vedastus Mwaria, Mwendesha Mashtaka, Zua Kawawa, alidai mtuhumiwa anadaiwa kutenda kosa hilo Januari 6, mwaka huu .

Katika kesi namba 203 ya mwaka 2020 iliyosomwa mahakamani hapo Agost 11, mtuhumiwa alikana shtaka hilo na la kumtumia mwanafunzi huyo kuosha vyombo nyumbani kwake kama ilivyodaiwa na mwendesha mashtaka. Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alikuwa akimtumia mwanafunzi huyo kuosha vyombo na kwamba siku ya tukio alimwita ndani kwake na kumbaka baada ya kuzima taa.

Hata hivyo mshtakiwa huyo alikana shtaka hilo.

Kesi hiyo imepangwa kusikilizwa Septemba 9, mwaka huu ambapo mashahidi kumi wa upande wa Jamhuri watahitajika kwenda kutoa ushahidi.

# NEC yafunga dirisha Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imefunga dirisha la uchukuaji fomu za kuomba kuteuliwa kugombea urais Ofisi ya Dodoma huku vyama 16 vikijitosa.

Vyama hivyo ni pamoja na Chama cha Mapinduzi (CCM) chenye mgombea wake Dk. John Magufuli, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, Chama cha AAFP, mgombea wake Seif Maalim Seif.

Wengine waliochukua fomu ambao vyama vyao vipo kwenye mabano ni Philipo Fumbo (DP), Leopold, Mahona (NRA), Muttamwega Mgaywa (SAU), Queen Sendiga (ADC), Twalib Kadege (UPDP) na Bernard Membe (ACT-Wazalendo).

Pia, wamo mgombea Cecilia Mmanga (Demokrasia Makini), Hashim Spunda (CHAUMMA), Khalfani Mazrui (UMD), David Mwaijolele (CCK), Prof. Ibrahim Lipumba (CUF), Yeremia Maganja (NCCR Mageuzi) na John Shibuda (ADA-TADEA).

Hata hivyo, kati ya vyama 19 vilivyosajiliwa, viwili vimetangaza kumuunga mkono mgombea wa CCM, ambavyo ni Chama cha TLP na UDP huku chama cha NLD kikitarajiwa kuchukua fomu jijini Dar es Salaam baada ya kufanya uteuzi wa wagombea wake wiki ijayo.

Akizungumza jana kuhusu zoezi hilo, Mkurugenzi wa Tume hiyo, Dk. Wilson Mahera, alisema tangu Agosti 5, mwaka huu, vyama 16 kati ya 19, vimechukua fomu hizo.

"Barua nyingine tuliyonayo ya chama cha 17 ambao watakuwa na mkutano wao wa uteuzi Agosti 16, mwaka huu, tumewapangia kama watajitokeza watachukulia fomu Dar es Salaam," alisema.

Alisema kwasasa wagombea hao wanatafuta wadhamini kwenye mikoa mbalimbali nchini na Agosti 25, mwaka huu, ndio siku ya uteuzi wa wagombea watakaokuwa wamekidhi masharti ya NEC.

Kati ya wagombea waliochukua fomu hizo wanawake ni wawili na upande wa Makamu wa Rais (Mgombea mwenza), wanawake ni watano.

"Agosti 22 hadi 25, mwaka huu, tutakuwa hapa Dodoma kwa ajili kupokea fomu na kuteua wagombea," alisema.

Kuhusu suala la mgombea binafsi, Mkurugenzi huyo alisema Tume hiyo inafanya kazi kwa kuzingatia sheria zilizopo na kwa kutumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Sifa za mtu kuwa Rais lazima awe raia wa kuzaliwa, awe mtu aliyeteuliwa na chama cha siasa kilichosajiliwa, kwasababu hilo ni takwa la Katiba na sheria, katika sheria na Katiba iliyopo hakuna suala la mgombea binafsi," alisema.

# Asakwa kwa tuhuma za kumnyonga mkewe

Na Gurian Adolf,
SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa, linamsaka Joseph Kalolo, maarufu kwa jina la mwamba, kwa tuhuma za kumuua mkewe kwa kumnyonga kutokana na kile kinachodaiwa ni wivu wa kimapenzi.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa Rukwa, Justine Masejo, tukio hilo limetokea juzi alfajiri saa 11:00, huku akimtaja mwanamke huyo aliyeuawa kuwa ni Maria Kaozya (30).

Alisema taarifa za kuuawa kwa mwanamke huyo zilithibitishwa na jirani mmoja wa familia hiyo aliyefika eneo la tukio asubuhi ya Agosti 8, mwaka huu, kumjulia hali. Baada ya kufika ndipo alipogundua kuuawa kwa mwanamke huyo.

Kamanda Masejo alisema chanzo cha mauaji hayo ni mgogoro wa kifamilia na kwamba muda mrefu wanandoa hao walikuwa katika mgogoro wa kimapenzi huku mke akidaiwa kutokuwa mwaminifu katika ndoa.

Alisema siku ya tukio, mwanamume alirudi usiku na kuanza kumpiga mwanamke hali iliyomsababishia majeraha kadhaa mwilini lakini kama haitoshi alimnyonga shingoni hadi kufariki dunia.

Baada ya kutenda unyama huo, Kamanda Masejo alisema, mtuhumiwa aliondoka na kwenda kusikojulikana hadi jirani huyo alipogundua asubuhi na kutoa taarifa polisi ambao walifika eneo la tukio na kuchukua mwili kwa ajili ya uchunguzi zaidi wa kitabibu.

Kamanda Masejo alisema polisi wanaendelea kumsaka mtuhumiwa huyo ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake.

Katika tukio lingine, mtu mmoja asiyefahamika katika eneo la Majengo mjini Sumbawanga, mwili wake umekutwa ndani ya pagala akiwa amefariki dunia.

Masejo alisema mwili wa mtu huyo ulikutwa juzi nyakati za asubuhi maeneo ya karibu na kilabu cha pombe za kienyeji na haikufahamika mara moja nini kimemsababishia kifo hicho.

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
## MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU VITUO VYA UTANGAZAJI NCHINI VINAVYOJIUNGA NA VITUO VINGINE VYA UTANGAZAJI VYA NDANI NA NJE YA NCHI NA RAIA WA KIGENI KUTEMBELEA VITUO VYA UTANGAZAJI HAPA NCHINI.

**1.0 UTANGULIZI**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ina dhamana ya kusimamia Sekta ya Utangazaji pamoja na Sekta nyingine za Mawasiliano, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa vituo vya Utangazaji vinazingatia weledi wa vipindi na habari au matukio yanayorushwa na vituo vyao. Ili kuhakikisha kuwa vituo vya Utangazaji vinatimiza wajibu wao, TCRA hutumia Kanuni zinazosimamia Sekta pamoja na kutoa leseni zilizo na msharti (Licence conditions) ya jinsi ya kutoa huduma za Utangazaji nchini.

**Kanuni ya 37** ya "THE ELECTRONIC AND POSTAL COMMUNICATIONS (RADIO AND TELEVISION BROADCASTING CONTENT) REGULATIONS, za 2018" ziliruhusu vituo vya Utangazaji kujiunga na kituo chochote cha utangazaji kwa ajili ya matangazo mubashara ili mradi kunakuwa na makubaliano ya kibiashara.

**2.0 UZOEFU ULIOPATIKANA**

Katika kusimamia utekelezaji wa Kanuni hii, kumekuwa na changamoto ya vipindi au habari zinazorushwa na vituo vya Utangazaji hasa pale vinapojiunga na vituo vya Utangazaji vilivyoko nje ya nchi na kurusha habari au matukio yanayohusu nchi yetu. Kwa mfano inapotokea dhahiri kuwa habari zinazohusu Nchi yetu hazikuzingatia maadili na weledi wa uandishi wa habari, huku habari hizo zikirushwa na vituo vilivyopewa leseni na TCRA, ni dhahiri hiyo inasababisha changamoto katika utekelezaji wa Kanuni hizo.

**3.0 UTATUZI**

Ili kuweza kusimamia vizuri maudhui ya nje yanayorushwa mubashara, Kanuni ya 37 ilifanyiwa marekebisho mwaka 2020 kwa kuongeza kanuni ndogo (2) inayokitaka Kituo chochote cha Utangazaji kinachotaka kujiunga na kituo kingine cha ndani au nje ya nchi kwa ajili ya kurusha matangazo yake yakiwemo yale ya mubashara kupata kibali/ruhusa ya kufanya hivyo kutoka TCRA. Huu ni utaratibu tu wa kawaida na biashara zitaendelea.

Aidha, ifahamike kuwa marekebisho haya yanavihusu vituo vyote vya utangazaji vya Redio na Televisheni na watoa huduma za Maudhui Mtandaoni (Online Radio & Televisheni).

Hivyo, TCRA inavielekeza vituo vya Utangazaji vinavyohitaji kurusha matangazo ya vituo vya Utangazaji vilivyoko nje ya nchi kuwasilisha makubaliano yao TCRA na kupata kibali kama utaratibu wa kawaida wenye lengo la kuleta ufanisi katika usimamizi wa maudhui yanayorushwa na vituo hivyo.

Kwa vituo ambavyo tayari wanarusha matangazo ya vituo hivi, vinatakiwa kuomba kibali/ruhusa husika na kuwasilisha makubaliano yao TCRA na sio kusimamisha matangazo au makubaliano yaliyopo. Huu ni utaratibu mzuri utakaoiwezesha TCRA kufahamu makubaliano hayo na kusimamia Sekta kwa ufanisi kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo.

Vile vile Kanuni ya 37 ilifanyiwa marekebisho pia mwaka 2020 kwa kuongeza Kanuni ndogo ya (4) inayotaka raia wa kigeni anayetaka kutembelea kituo cha Utangazaji kwa shughuli inayohusiana na utangazaji au kufanya biashara/shughuli inayohusiana na utangazaji kuambatana na Afisa wa Serikali au wa TCRA. Kwa mantiki hiyo Kituo cha Utangazaji hakiruhusiwi kumruhusu raia wa kigeni kwa shughuli zilizotajwa kama hajaambatana na Afisa husika.

**Kanuni hii ya 37 (4) imewekwa ili:**

i. kuweka uwazi madhumuni ya ushiriki wa raia wa kigeni katika shughuli za utangazaji wanapotembelea vituo vya Utangazaji hapa nchini;
ii. Kutimiza matakwa ya itifaki za kidiplomasia kuwa wawakilishi wa nchi za nje na mashirika ya kimataifa wanapaswa kuambatana au kupokewa kule wanakokwenda na maafisa wa Serikali wanapokuwa wamepata kibali cha kutembelea miradi ambayo wanajihusisha nayo; na
iii. Kuhakikisha uendeshaji wa vituo vyetu vya utangazaji unazingatia udhibiti wenye uwazi (Regulatory Monitoring Transparency) hususan kwa upande wa ufundi maana ujenzi wa vituo hivyo huruhusiwa kwa kibali (Construction Permit – CP) cha TCRA.

Kwa hiyo, TCRA inavielekeza Vituo vyote kuwasilisha maombi yao ndani ya siku saba (7) tokea kutolewa kwa Taarifa hii kwa mara ya kwanza 11 Agosti, 2020. Na, tunawashukuru wale ambao tayari wameanza kutekeleza wito huu.

Ifahamike pia kwamba hoja kuu hapa ni Vyombo vya Habari na si Waandishi wa Habari.

**Imetolewa na:**

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,**
**Mawasiliano Towers,**
**Kitalu Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,**
**S. L. P 474,**
**14414 DAR ES SALAAM**
**12 Agosti, 2020**

215856202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mameneja TANESCO watii agizo la waziri umeme kutokatika

**KUKATIKA** kwa umeme kila wakati katika baadhi ya maeneo nchini bila kuwapo sababu za msingi, ni moja ya kero ambazo zimekuwa zikilalamikiwa na wananchi.

Nishati ya umeme ni huduma muhimu sana inayogusa maisha ya kila mtu, kwa sababu bila umeme mambo mengi hayawezi kwenda. Kukosekana kwa huduma hiyo kunasimamisha karibu shughuli zote za majumbani, shughuli za biashara na viwandani.

Kwa lugha rahisi unaweza kusema umeme ni kila kitu na kukosekana kwake hakuna maisha.

Kero ya umeme imekuwapo kwa miaka mingi, ingawa serikari zote tangu Uhuru kila moja imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuhakikisha wananchi wanapata umeme katika maeneo yote ya mijini na vijijini. Katika kuhakikisha kwamba huduma za umeme zinazogezwa karibu ili kila Mtanzania popote alipo apate na kunufaika na huduma hiyo, serikali ilianzisha na kuanza kutekeleza mradi wa umeme vijijini, ambao unatekelezwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA).

Hilo ni moja ya mafanikio ambayo serikali hainabudi kujivunia kwa kuwa inaelezwa kuwa vimebakia vijiji takribani 3,000 nchi nzima ambavyo havijapata nishati hiyo, ingawa jitihada zinaendelea kuhakikisha kila kijiji kinafungiwa nishati hiyo.

Hata hivyo, yamekuwapo malalamiko ya kila mara ya kukatika kwa umeme mara kwa mara, hivyo kuwaathiri wananchi kufanya shughuli mbalimbali hususan za kujipatia kipato.

Malalamiko hayo yamekuwa yakitolewa kwa viongozi wa serikali wanapofanya ziara kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme nchi nzima. Kutokana na hali hiyo, wiki chache zilizopita, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alikemea tabia hiyo na kuwapa angalizo mameneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuhakikisha kwamba kero ya kukatika umeme ovyo inapatiwa ufumbuzi.

Katika kuonekana amekerwa na hali hiyo, Waziri Kalemani aliwataka mameneja hao kujitathmini na kuelekeza kuwa kukatika kwa umeme kitakuwa moja ya vigezo vya kupima utendaji wao.


Katika mazingira ya sasa ambayo mawaziri wamekuwa wakisimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi iliyoko chini ya wizara zao, ulikuwa uamuzi sahihi wa Dk. Kalemani wa kuwapa mameneja hao angalizo hilo kama njia ya kuwajibika kwao.

Haiwezi kueleweka mawaziri akiwamo Dk. Kalemani wahangaike kupita maeneo yote ya nchi kukagua miradi inayotekelezwa halafu watendaji walioko chini yao washindwe kuwajibika kwa kutatua kero za wananchi ambazo ziko chini ya uwezo wao kama kukatika umeme ovyo. Watendaji hao hawanabudi kuweka utaratibu wa kufuatilia kero za wananchi, ikiwamo kuwaendea na kuwapa maelezo kuhusu sababu za kukatika kwa umeme na ni hatua gani zinachukuliwa kupata ufumbuzi.

Sote tunaelewa kuwa kukatika kwa umeme ni jambo lisilozuilika katika mazingira ya nchi yetu ambayo haijapata umeme wa uhakika kwa asilimia mia moja, lakini basi lazima wahusika watoe taarifa kwa wananchi ili wajiandae. Kuna maeneo kadhaa kama ya Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani na kwingineko ambako wananchi wanalalamikia kukatika umeme kila wakati hususan siku za Ijumaa na Jumamosi bila taarifa. Ikumbukwe kuwa wakati huu ambao Tanzania imedhamiria kuingia katika ujenzi wa viwanda, umeme ndio tegemeo kuu ya kukidhi hitaji hilo, hivyo kuna haja ya wahusika wa TANESCO kuweka utaratibu wa kuhakikisha wawekezaji na wajasiriamali wanakuwa na umeme wa uhakika.

Pale linapotokea tatizo, basi zitolewe mapema, badala ya kuwaacha watumiaji wasijue kinachoendelea, na kuathiri shughuli zao. Tunakubaliana na Waziri Kalemani kwamba kutokatika kwa umeme kiwe kigezo cha kupima utendaji wa mameneja wa shirika hilo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kulikoni vijana tunakumbatia corona na kuutelekeza Ukimwi?

Na Sabato Kasika

**ELIMU** ya saikolokojia wanayofunzwa matabibu, inaeleza tabia ya hofu ya binadamu, hupitia madaraja kadhaa. Mwanzo anapofahamu jambo baya dhidi yake, hukumbwa na hofu na woga uliopitiliza wa kutokukubaliana nayo hata kidogo.

Baada ya hapo, huanza kuikubali katika mtazamo wa hofu iliyobebwa na mtazamo wa mazoea ya mbali yakibebwa na msamiati 'itakuwaje?' Kisha baada ya hapo, anakubaliana nayo ama kwa masharti ya upande wake au kutoka adui hofu akijipa moyo 'sawa twenda nayo hivyo hivyo'.

Hicho ndicho kinachotarajiwa hata kwa mgonjwa anayepewa taarifa rasmi, mathalani umefikiwa uamuzi wa kitabibu ni kwamba, lazima hakuna namna mkono au mguu ukatwe.

Mtazamo mkuu, ndiyo uliotawala kwa jamii nchini mwanzoni mwa miaka ya 1980, baada kuingia taarifa za kuwapo kwa ugonjwa wa Ukimwi kwa jamii ya Kitanzania, kwa kiasi kikubwa sehemu kubwa ya umma, ilikinga sikio kwa wakazi wa mkoa wa Ziwa Magharibi, au kwa msamiati waujuao vijana wa leo, Mkoa wa Kagera.

Haikuchukua safari ndefu ikawa janga la kitaifa na vita vya kuvikabili vikawa vya kitaifa, hofu yake ikipitia awamu zote na sasa tumegota katika 'sawa twenda nayo hivyo hivyo'.

Siyo sisi peke yetu, bali dunia kwa jumla, chini ya mratibu Shirika la Afya Duniani (WHO), linaumiza ubongo wa namna ya kuvikabili, Insha-allah angalau hatua imepigwa tunapuma na kuendelea kuwaona wenzetu kwa msaada wa ARV.

Tukiwa hapo hapo kwenye 'sawa twenda nayo hivyo hivyo', ameibuka binamu yake Covid-19 na aliyoyatenda duniani, hakuna haja ya kusimuliana. Kwa mara nyingine, vita vyetu na juhudi za maombi Insha-allah kwa mara nyingine aliye mkuu ametutendea, walau tunapumua.

Lakini hapo nina maoni. Ninaona kama kuna dalili ya kisaikolojia, baadhi yetu tunamfanya anayetumezesha ARV tunampa hadhi ya malaria, eti tishio kwetu ni huyu corona. Jamani jamani, tuteme mate chini! Bado yupo palepale!

Walengwa wangu hasa, ni wenye damu inayochemka- vijana, warejeshe kumbukumbu nyuma namna ilivyoangamiza si kwetu tu, simulizi ni ya dunia.

Viongozi wanaotunza takwimu zetu kuu, wanatuambia kuna maambukizo mapya ya virusi vya Ukimwi kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 na dawa kuu kwa jamii hiyo ambayo ni nguvukazi tegemezi kitaifa. Jamani, tubadilike haraka ikiwezekana, leo leo!

Tunaambiwa maambukizi mapya kwa vijana ni asilimia 40. Pia tukilichukua kundi hilo hilo, wenye jinsi ya kike 'walioumia' ni asilimia 80 au kwa lugha rahisi ni robo tatu na ushee.

Nikilainisha hisabati hizo, ninaona kwamba asilimia 32 ya 'walioumia' kupitia janga hilo ni hawa mama zetu katika umri mdogo.

Nadiriki kukubaliana na hoja kwamba, wao wako hatarini zaidi. Waziri mwenye dhamana na Afya, Ummy Mwalimu, alilazimika kuanika uhalisia huo katika mizunguko yake kikazi, mahsusi akikagua huduma na ujenzi unaoendelea katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Katavi.

Ummy anakumbusha hatua ya Bunge ilivyorasimisha Sheria ya Wananchi Kujipima Wenyewe Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU). Kwa kifupi anamaanisha, ni ruksa kujipima maambukizi hayo, vifaa vya kazi hivyo navyo ni ruksa kupatiwa wananchi iwe kwa mauzo katika maduka ya dawa au kwa namna nyingine yoyote rasmi.

Nami nichangie hoja, jamani ndugu zangu wa 'NGO' na wengineo wanaojiweza 'fanyeni mambo' sheria iwafikie kwa matendo Watanzania wote. Tutakuwa tunadanganyana, tukibananisha saikolojia yetu na hofu ya corona na kisha VVU tunaiweka katika kapu la malaria na kuharisha. Hiyo ni sawa na masihara wanayotumia wapenzi wa soka kwamba 'mlinzi ameenda kuzurura, wakati kuna hatari golini kwake na mlinda mlango naye hayupo.'

Kielimu inaelezwa, panapoonekana maarifa yanalegea, huenda kuna kulegea kwa elimu, pamoja na itikadi na falsafa yake. Kama ndiyo hivyo, wadau washika usukani, kazeni kamba kupitia elimu inayojitosheleza, maarifa ya kina kuhusu ugonjwa huo, yapenye kila mahali.

Si mbaya kujiuliza swali nafasi ya umaskini, sera na mikakati ya kila siku imekaa sawa sawa? Maana bado tunashuhudia vijana na ngono zembe, maskini ya Mungu wengine ukiwaona usoni, umri miaka 15 au chini ya hapo nao wanaangukia ama hatarini au wameshakumbwa na adha ya VVU.

Najua kuna wanaodanganywa na maumbo kukua zaidi ya umri, uzembe na uelewa duni wa wazazi na walezi na mengine mengi ya namna hiyo.

Hata hivyo nakiri, kuwapo kwa Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti Ukmwi 2018/19 - 2022/23 unaolenga kupunguza maambukizi mapya ya VVU kwa asilimia 75 kufikia mwaka huu na asilimia tano kwa watoto wetu ifikapo mwaka 2023. Swali kuu tujiulize, tunaendeleaje?

MAKALA


# Mkapa alilenga kujenga Ujamaa katika mazingira mapya

**Na Waandishi Maalum**

**SEHEMU ya tatu na ya mwisho ya ushuhuda wa Mzee FERDINAND Kamuntu Ruhinda juu ya rafiki yake wa zaidi ya miaka 50, Benjamin William Mkapa, Rais wa tatu wa Tanzania, aliyefariki dunia Julai 23 na kuzikwa Julai 29, mwaka huu, kijijini kwao, Lupaso, Mtwara. Endelea kusoma......**

BENJAMIN William Mkapa alikuwa muumini wa dhati wa mambo makubwa kadhaa ambayo ndiyo yalikuwa falsafa kuu na misingi mikuu ya urais wake na uongozi wa Tanzania kwa miaka 10, na hata kabla ya kuingia madarakani.

Kwanza, alikuwa mwanafunzi na mfuasi mwaminifu wa Mwalimu Nyerere. Pili, alikuwa muumini wa Sera ya Uwazi na Ukweli. Tatu, aliamini katika ujenzi wa uchumi wa kisasa, kama njia ya uhakika na kisayansi kuwatoa watu katika umasikini. Nne, alichukia unyonyaji wa mtu kwa mtu. Tano, aliamini katika uongozi wa pamoja na alichukia mno tashihisi, yaani tabia ya kuabudiwa (personality cult). Sita, aliamini kuwa nchi haiwezi kujengwa kwa misingi ya kusadikika na kufikirika (utopia).



Benjamin Mkapa akihutubia katika moja ya mikutano yake.

Hivyo ndivyo Balozi Ruhinda, rafiki wa karibu wa kimaisha, kifamilia na kisiasa wa Mkapa kwa zaidi ya miaka 50, anavyoeleza, kwa ufupi tu, misingi mikuu iliyomwongoza Hayati Mkapa katika uongozi wake.

"Benjamini Mkapa alikuwa muumini na mwanafunzi wa Mwalimu Nyerere, kama tulivyokuwa Watanzania wote. Lakini hakuwa mwanafunzi wake wa darasani (siyo kweli kuwa Mwalimu alimfudisha Mkapa pale Pugu. Mkapa aliingia Pugu wakati Mwalimu anajiuzulu ama amejizulu kazi ya ualimu). Hivyo, uanafunzi wa Ben kwa Mwalimu ni wa siasa, tabia na uongozi."

"Kubwa hapa ni kwamba Benjamin Mkapa alikutana na Mwalimu mapema sana katika maisha yake, mara tu baada ya masomo yake, na akafanya kazi naye kwa miaka mingi, na akawa muumini wa kiongozi huyo, ambaye aliamini katika Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, "anasema Mzee Ruhinda na kuongeza:

"Na kama tunavyojua, Mwalimu alilenga kujenga Ujamaa wenye misingi ya Utamaduni wa Kiafrika. Hii ilikuwa tofauti na baadhi ya watu walivyoamini kuwa Ujamaa lazima ujengwe kwa kupambanisha matabaka ndani ya jamii. Sasa nyie mnajua kuwa binafsi nimeishi na kutembelea baadhi ya nchi za nje ambazo nyingine zilijenga ujamaa – China, Sweden, Korea Kaskazini, Cuba na pia nilikaa Canada. Moja ya mambo niliyojifunza ni kwamba katika nchi zote, hakuna kiwango kilicho sawa (Standard) cha ujenzi wa Ujamaa."

"Korea Kaskazini kule sijui hata wanajenga Ujamaa wa namna gani. Cuba wao wako katika mapambano yao ya miaka mingi na Marekani. Sweden ni sehemu ya nchi za Scandnavia ambazo zina mfumo wa dola la ustawi (welfare state). China wao wanajenga Ujamaa wenye sifa za Kichina (socialism with Chinese characteristics)...Sasa utaona kuwa hakuna Standard moja ya ujenzi wa Ujamaa duniani."

Anafafanua Balozi Ruhinda: "Bwana Mkapa naye, kama nilivyosema, alikuwa muumini na mwanafunzi wa Mwalimu, na kama alivyokuwa Mwalimu, Ben alichukia unyonyaji wa mtu kwa mtu, hata kama alijua kuwa binadamu lazima wawe tofauti. Lakini tofauti zile zisitokane na kundi moja lenye uwezo kuwanyonya wasiokuwa nacho. Aliamini katika jamii sawa, na alilenga kujenga usawa miogoni mwa Watanzania."

"Kwa maneno mengine, Ben alijitwisha mzigo wa kujenga Ujamaa lakini katika mazingira mapya ya Tanzania na kwa kutilia hali halisi ya nchi yetu. Hii ni sawa zilivyofanywa ama zinavyofanya nchi nyingine nilizozitaja hapo juu katika kujenga Ujamaa, kila nchi katika mazingira na hali halisi yake."

"Ben, kama ilivyo siasa yetu ya Ujamaa, alipinga sana unyonyaji na alilenga kujenga usawa miongoni mwa watu. Falfasa yake na hatua zake zote zililenga kufanikisha hayo mawili – kufuta umasikini na kujenga usawa katika nchi yetu. Huu ndiyo msingi wa kuundwa kwa taasisi kama TASAF, na kubuniwa kwa Programu kama vile Dira ya Maendeeo ya 2025 na kuwekwa kwa misingi ya uchumi wa kisasa," anafafanua Mzee Ruhinda.

Mzee Ruhinda anaelezea kuwa katika kufanikisha lengo la kuwatoa watu katika umasikini, ambalo pia ndiyo lilikuwa lengo kuu ya Siasa ya Ujamaa, Mkapa alibuni mbinu mbalimbali za utekelezaji wa azma hiyo kwa sababu alijua fika kuwa ilikuwa vigumu sana kujenga Ujamaa kwa fikra tu, kwa Utopia (njozi) ama kwa njia ya kufikirika na kusadikika.

Moja ya mbinu hizo za kutimiza lengo la kuondoa umasikini, anaeleza Mzee Ruhinda, ilikuwa ni kujenga misingi ya uchumi wa kisasa ambao faida zake zingesambaa haraka kwa watu wengi zaidi. Anasema Balozi:

"Rais Magufuli amelizungumzia vizuri sana hili...alitoa hotuba nzuri sana pale uwanjani, na Rais Kikwete ameyarudia yale yale vizuri sana pia katika hotuba yake kule Lupaso wakati wa mazishi ya Ben. Wote wamezungumza kwa kina jitihada za Ben kuweka misingi ya ujenzi wa uchumi wa kisasa. Lakini katika ujenzi wa misingi ya uchumi huo wa kisasa, ilibidi achukue hatua nyingine, hata kama hatua hizo zilizua maneno mengi, kama kubuni na kutekeleza Sera ya Ubinafsishaji."

"Zipo hatua nzuri nyingi ambazo Mwalimu Nyerere alizichukua, lakini utekelezaji ukawa unashindikana, kwa sababu ya hali halisi ya Tanzania, kama vile kutaifisha mashamba na viwanda, na kuunda mashirika ya umma lukuki, yote yakibebwa na kodi ya wananchi. Sasa wapo watu waliomlaumu sana Mkapa kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha Duniani (IFM). Ushirikiano na mashirika hayo hakuwezi kuzuia ujenzi wa Ujamaa, na jamii ya usawa na haki. Leo ukienda China ama Urusi huwezi kusema nchi hizo hazijengi Ujamaa kwa sababu nazo zinashirikiana na mashirika hayo makubwa ya kimataifa ya fedha na uchumi."

"Kama ambavyo Ujamaa usingeweza kujengwa kwa kufikirika (Utopia) vile vile uwekaji wa misingi ya uchumi wa kisasa. Ili kufanikisha mageuzi hayo ya kiuchumi, Ben alilazimika kuangalia mazingira ya nchi na kufanya mabadiliko ya msingi, ili kujenga msingi wa mageuzi yenyewe. Kama nilivyosema hapo mapema, Mkapa alijitwisha mzigo wa kuendeleza fikra za Ujamaa katika mazingira mapya ya Tanzania."

Balozi Ruhinda anageukia suala jingine la msingi katika utawala wa Rais Mkapa na kusema: "Kweli, Mkapa aliweka misingi ya uchumi wa kisasa, lakini hakuwa peke yake katika kuifanya kazi hiyo. Ilikuwa ni Mkapa akifanya kazi na watu wengine – alikuwa na mawaziri wake na Baraza lake la Mawaziri, alikuwa na chama chake, alikuwa na Benki Kuu ya Tanzania na watu wengine wengi. Dira ile ya maendeleo ya 2025, sijui sasa imefikia wapi, aliibuni na watu wengine. Kwa hiyo, mafanikio yote haya hakuyaleta Mkapa peke yake. Yeye mwenyewe aliamini fika katika uongozi wa pamoja."

"Tuna tatizo kubwa sana la tashihisi (personification) ya mambo, na tabia ya kujenga abudu kwa viongozi (personality cult). Utaratibu huu wa personalization unaendelea sasa, lakini ni hatari kujenga abudu katika mambo ya uongozi. Ni kweli, tunahitaji awepo kiongozi, lakini kiongozi siyo kila kitu. Kwa mfano, tunajisifu sana kuhusu nchi kuingia uchumi wa kati. Mimi sijasoma popote, lakini nasikia Benki ya Dunia ndiyo imetangaza kuwa tumeingia uchumi wa kati. Lakini tukumbuke kuwa huo ni mwanzo tu. Ndio kwanza tumefungua milango ya uchumi huo wa kati. Tusijisifu sana kupita kiasi. Safari ya kukamilisha hili na kuwatoa Watanzania katika umasikini bado ndefu."

Balozi Ruhinda pia anazungumzia nafasi ya Mkapa kama mwandishi wa habari na mhariri wa magazeti na kusema: "Wakati najiunga na The Nationalist, na nyinyi wenyewe mmefanyakazi katika vyombo vya habari na mnajua utaratibu huu, tulikuwa tunafanya mikutano ya tathmini ya magazeti kila siku asubuhi. Yeye ndiye alikuwa mwenyekiti wa mkutano huo. Tulijadiliana kwa uwazi, kwa urafiki na uhuru kamili kama wanataaluma. Tulikubaliana na tulihitilafiana. Lakini hatimaye, yeye kama Mhariri ndiye alitoa msimamo wa mwisho. Na kwa kweli hiyo ndiyo kazi ya Mhariri kutoa msimamo na mwelekeo wa gazeti. Kwa maana hiyo, Mhariri yeyote ni Mdhibiti wa gazeti lake."

Anaongeza Balozi Ruhinda: "Lakini kwa maana ya kwamba yeye Mkapa aliwazuia waandishi kuandika walivyotaka kulingana na sera ya gazeti, ama alizima mawazo yao, hapana, na wakati ule gazeti lile lilikuwa na waandishi kutoka Ghana, kutoka Biafra. Isipokuwa, ni kweli kuwa uamuzi wa mwisho ulikuwa wa kwake, akiwa Mhariri, kama walivyo wahariri wengine wowote duniani."

Balozi Ruhinda pia anasema kuwa siyo kweli kuwa Mkapa aliletwa kuongoza gazeti bila kuandaliwa ama kusomea na kupata uzoefu wa kazi na taaluma ya uandishi wa habari.

"Mkapa vile vile alipata mafunzo ya uandishi wa habari," anasema Mzee Ruhinda na kufafanua: " Kabla ya kujiunga na vyombo vya habari, Ben alipelekwa kwenye Gazeti la (Daily) Mirror, Gazeti kubwa na maarufu la Uingereza, na kufanya kazi kule kwa muda, akipata mafunzo kama mwandishi wa habari na kuandaliwa kuwa Mhariri."

Lakini hata kabla ya kupelekwa Gazeti la Mirror, Ben alikuwa na uwezo mkubwa wa kuandika na kuhariri. "Kwa maoni yangu, Ben alikuwa mwandishi wa habari na Mhariri mzuri."

"Nimalizie, kama nilivyoanza mahojiano haya, kwa kusema: Nilimpenda Ben kwa sababu ya utu na ubinadamu wake. Kama nilivyoeleza, Ben alikuwa na sifa zote nzuri ambazo binadamu anastahili kuwa nazo. Ni binadamu aliyeongozwa na fikra na nia njema wakati wote katika maisha yake. Buriani, Benjamin William Mkapa, rafiki yangu, ndugu yangu."

**■ Makala hii imeandikwa na waandishi waandamizi nchini. Salva Rweyemamu na Saidi Nguba, kwa sasa wanaongoza Kampuni ya Mawasiliano ya Pioneer Communications, na Tido Mhando ni Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya habari ya Azam Media.**



Abiria wa daladala na bajaj wakitembea kuelekea Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam, baada ya kutokea foleni ya magari iliyodumu kwa zaidi ya nusu saa katika barabara ya Morogoro, eneo Kibanda cha Mkaa, jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mwigulu awataka wasajili watoto kuwa waadilifu

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SERIKALI imewataka wasajili wanaotoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto kuweka uzalendo mbele kwa kuhakikisha watoto wanaosajiliwa ni wanaostahili.

Pia, aliwataka wanaotoa vyeti hivyo kuhakikisha vinatolewa bure na kutotumia fursa hiyo kujipatia kipato.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema hayo katika hafla ya uzinduzi wa Mpango wa Usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto walio na umri wa miaka mitano katika mikoa ya Tanga na Kilimanjaro, iliyofanyika katika Uwanja wa Mandela eneo la Pasua, Manispaa ya Moshi.

Alisema mpango huo unatekelezwa kwa kusogeza huduma karibu na makazi ya wananchi kwa kuwa huduma zitapatikana katika Ofisi za Watendaji Kata na vituo vya tiba bila malipo.

Alieleza kuwa mpango huo ni muhimu kwa kuwa unatoa fursa kwa watoto kupata haki zao za msingi za kutambuliwa na kusogezwa kwa huduma itawafikia watoto wengi zaidi.

Aliipongeza RITA na wadau wengine kwa kufanikisha mpango huo ambao una umuhimu kwa serikali kwa kuwa utaiwezesha kupata takwimu kwa wakati kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo.

Mpango wa usajili wa watoto unatekelezwa na serikali kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ambao ni Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto Duniani (UNICEF), Serikali ya Canada na Kampuni ya Simu ya Tigo.

Katika utangulizi, Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu wa RITA, Emmy Hudson, alisema mafanikio makubwa yamepatikana na kuifanya Tanzania kuwa moja ya nchi ya mfano katika masuala ya usajili.

Katika Maadhimisho ya Siku ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu mwaka huu ambayo itafanyika kwa njia ya mtandao, Tanzania ni moja ya nchi tano za Afrika na pekee katika Afrika Mashariki zilizochaguliwa kuwasilisha mada ya jinsi ilivyofanikisha usajili katika kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu (Covid-19).

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya RITA, Prof. Hamis Dihenga, alisema mpaka sasa mpango huo umeanza na unaendelea kutekelezwa katika mikoa 16 ya Tanzania Bara na kuonyesha mafanikio makubwa, kusajili watoto 4,583,000 na kupata vyeti vya kuzaliwa na kuwataka wananchi wa mikoa ya Kilimanjaro na Tanga kuchangamkia fursa hiyo. Zaidi ya watoto 584,658 wanategemewa kusajiliwa katika mikoa hii miwili.

Alisema mafanikio ya mpango huo yanachangiwa na matumizi ya Teknolojia ya Mawasiliano kwa simu janja kutumika kutuma taarifa za wanaosajiliwa.

Watoto 623 walisajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa.

# Wasafiri Kilimanjaro Ferries sasa kulipia tiketi kidijitali

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wa Zantel watanunua tiketi za usafiri wa boti za Azam kwa njia ya Ezypesa baada ya kampuni hiyo kuingia ubia na kampuni ya usafirishaji ya Kilimanjaro Fast Ferries Ltd inayotoa huduma za usafiri wa boti.

Kampuni hiyo ni moja ya watoa huduma za usafiri wa majini kati ya Zanzibar na Dar es Salaam ikiwa na boti nne zinazochangia katika urahisishaji wa huduma za usafiri kwa wenyeji na wageni.

Mkuu wa Masoko na Huduma za Kifedha wa Zantel, Sakyi Opoku. alisema hatua hiyo imelenga kurahisisha upatikanaji wa huduma za ukataji tiketi kwa abiria, hivyo kuboresha maisha ya wateja wao.

"Kupitia Ezypesa tunahakikisha wateja wanafanya malipo yao kwa urahisi zaidi, mahali popote na wakati wowote. Ushirikiano wetu na Kilimanjaro Fast Ferries unawapa wateja uhuru wa kununua tiketi na kupunguza muda na mchakato wa kununua tiketi," alisema Opoku.

Ili kupata huduma hiyo, mteja wa Zantel atapiga namba ya Azam bure 0800 785 555 na atapewa namba ya kumbukumbu ya malipo na kisha atakwenda kwenye menyu ya Ezypesa *150*02# na kuendelea na malipo. Baada ya hapo ataingiza namba ya Kampuni 777444 kisha kumbukumbu namba, kiasi na mwisho kuthibitisha malipo.

"Tunaamini njia hii ni suluhisho na itaboresha namna wateja wanavyopata huduma za usafiri hususan wasafiri wa ndani kwani kwa sasa hakuna haja ya kwenda tena katika ofisi bali ukiwa na simu yako tu unaweza kujihakikishia uhakika wa kupata usafiri," alisema Opoku.

Mkurugenzi Mtendaji wa Azam Marine Ltd, Abubakar Salim, alisema kampuni hiyo imewekeza katika mifumo ya malipo mtandaoni ambayo inatumika duniani kote, ambayo imesaidia kuboresha upatikanaji wa huduma za usafiri.

"Ushirikiano baina yetu na Ezypesa umetanua wigo wa njia za malipo ambazo zinampa mteja uhuru wa kununua tiketi mahali popote alipo, wakati wowote bila malipo ya ziada," alisema Salim.

Wateja watakaofanya malipo kwa Ezypesa watachukua tiketi zao katika ofisi za Azam Marine siku ya kusafiri na watatakiwa kuonyesha ujumbe (SMS) ya uthibitisho wa malipo.

# SIDO yaibua viwanda 8,477 kwa miaka mitano

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwanda Vidogo (SIDO) limesema katika miaka mitano iliyopita limesimamia ujenzi wa jumla ya viwanda 8,477, ambavyo vimeibua zaidi ya ajira 500,000, hivyo kuchangia kukua kwa pato la taifa na kuifanya Tanzania kuwa taifa lenye uchumi wa kati.

Mkurugenzi Mkuu wa SIDO, Prof. Sylvester Mpanduji, alisema jijini Dar es Salaam kuwa uchumi wa kati umefungamana mno na kuwapo kwa viwanda, na kwamba SIDO imetekeleza kwa vitendo sera ya kuanzishwa kwa viwanda ili kufikia lengo la uchumi wa kati.

"Tumepata viwanda vikubwa 201, viwanda vya kati 460, viwanda vidogo 3406 na viwanda vidogo sana 4410 vimeanzishwa katika kipindi cha serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli na kuliwezesha shirika kufikia asilimia 98 ya malengo yetu," alisema Prof. Mpanduji

Alieleza kuwa viwanda vya ndani hurahisisha na kuboresha maisha ya watu kwa kuibua masoko ya malighafi, bidhaa za viwandani na ajira, hivyo kupunguza umaskini wa kipato.

Prof. Mpanduji alisema soko endelevu na lenye uhakika ni soko la ndani ya nchi, na kueleza kwamba SIDO inawahamasisha wazalishaji wa ndani kuzalisha bidhaa zenye ubora ili Watanzania wapende kununua bidhaa hizo. Amesema ni kwa njia hiyo Tanzania itaweza kuimarisha soko la ndani na kulinda viwanda vyake.

"Mteja anapenda kupata bidhaa bora kulingana na fedha yake. Hivyo ili viwanda ziendelee kuwapo, lazima ubora wa bidhaa uimarishwe ili kujenga imani ya wateja katika soko la ndani na hatua ya pili ni kuibua fursa ya kupata masoko ya nje ya nchi," alieleza.

Alisema ajira nyingi zimezalishwa na viwanda vidogo sana na viwanda vidogo, na kufafanua kuwa sekta ya viwanda imechangia asilimia 8.5 katika pato la taifa mwaka 2019, na kwamba mchango huo wa viwanda umehamasisha na kuchochea maendeleo nchini.

"Uwekezaji katika sekta ya viwanda, hususan viwanda vidogo nchini, umeongeza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ikiwamo bidhaa za nguo na mavazi na bidhaa za ngozi, kusindika nyama, chakula, mboga na matunda, maziwa, mafuta ya kula, sukari, vifungashio, mbolea, pamoja na viwanda vya kubangua korosho", alisema.

Ameeleza kuwa, katika kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa Corona, SIDO ilihakikisha viwanda vinazalisha vifaa vya kujikinga na ugonjwa huo ikiwamo utengenezaji wa barakoa na vifaa vya kujikinga.

"Vita dhidi ya Corona imekuwa rahisi kutokana na kuwapo kwa viwanda vyenye uwezo ndani ya nchi na upatikanaji wa bidhaa mbalimbali. Hali hii imepunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje ya nchi," alisema Prof.Mpanduji

Prof.Mpanduji alisema kuna ushirikianao kati ya SIDO na NSSF, VETA, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) na Azania Bank katika kuwawezesha wananchi kupata mafunzo ya ujasiriamali na mikopo.

HABARI KITAIFA



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, akiwa amemfunga pingu kijana muosha magari baada ya kuendesha gari bila ya kuwa na leseni na kusababisha ajali kwa kuigonga bajaj, eneo la Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NGO zaagizwa utoaji taarifa

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

MASHIRIKA yasiyo ya kiserikali yametakiwa kutoa taarifa za kazi zao kwa jamii ili kutimiza lengo lake la kuisaidia Serikali kutekeleza miradi ya kuhudumia wananchi.

Hayo yamesemwa na Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Kigoma , Samuel Tenga wakati wa kikao cha pamoja na Mashirika hayo na timu ya ufuatiliaji kutoka Ofisi ya Msajili wa NGOS.

Amesema lengo kuu la kuanzisha Mashirika siyo tu kujitafutia ajira, bali ni kuangalia pengo lililopo katika kuhudumia wananchi.

"Lengo ni kuangalia pengo ili kuhudumia wananchi, kuna mashirika ambayo yanapata ufadhili, lakini changamoto ni mawasiliano kati ya mashirika hayo na Serikali ngazi ya halmashauri hadi mkoa kutokuwa mazuri," alisisitiza.

Alisema kwa uzoefu wa Mkoa wa Kigoma, mawasiliano yamekuwa siyo mazuri kwani kati ya mashirika 150 yanayotambuliwa, yanayotoa taarifa si zaidi ya mashirika 10.

"Ni changamoto kwa sababu Serikali ya mkoa au wilaya inatakiwa ijue wadau wake na mchango wake kwa wananchi, kuna suala la kutoa taarifa za miradi inayotekelezwa ila umekuwa na pengo la kutoa taarifa" alisema.

Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini Mwandamizi kutoka Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Musa Leitura, alisema Serikali inatambua mchango wa mashirika katika kuhudumia wananchi.

"Tumetembelea baadhi ya mashirika, tumekuta miradi inaridhisha, kwa maana hiyo tunatambua mnafanya kazi kubwa kuisaidia Serikali," alisema.

Ameongeza kuwa baadhi ya upungufu uliobainika katika kufuatilia mashirika hayo ni kutokuwa na ofisi, kutowasilisha taarifa kwa Msajili, kutokuwa na mpango wa uendelevu wa mradi na kutolipa ada.

# Wahofia majitaka kwenye mitaro ya maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wilayani Kahama, Mkoa wa Shinyanga, wako hatarini kupata magonjwa ya mlipuko kutokana na baadhi yao kuunganisha mifumo ya majitaka kutoka kwenye mitaro inayopitisha maji barabarani.

Walisema hayo jana wakati wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti na kubainisha kuwa mitaro yote inayopitisha maji wakati wa mvua za masika hasa iliyopo maeneo katikati ya mjini kutitirisha maji machafu na kuwatia hofu wananchi kupata magonjwa ya mlipuko.

Denis Kasindi, mkazi wa kijiji cha shunu Kata ya Nyahanga, alisema kama idara ya afya na mazingira ya Halmashauri haitachukua hatua dhidi ya wanaounganisha mifumo ya majitaka hadi kwenye mitaro ya barabara, basi magonjwa ya mlipuko kama kuhara damu, kichocho na kipindupindu hayataisha.

Aliongeza kwamba ugonjwa wa corona pia utaendelea kuishi katika mazigira yao.

Nae Zuhura Juma, mkazi wa Kata ya Majengo, alisema idara ya mazingira inatakiwa kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira na usafi sambamba na kuwachukulia hatua za kisheria wote waliunganisha mifumo ya majitaka na mitaro ya maji na kutiririsha maji hayo.

"Maji machafu wakati wa mvua za masika yanajaa majitaka na kusababisha mitaro kuwa mweusi na watoto wanashinda wanachezea maji hayo, hivyo kutishiwa kuugua magonjwa ya mpuliko ambayo ni hatari kwa afya zao," alisema Juma.

Akijibu hoja hiyo, Ofisa Mazingira wa Halmashauri hiyo, Johanes Mwebesya, alisema zaidi ya wakazi 100 wametozwa faini baada ya kubainika kuunganisha mifumo ya majitaka na kuelekeza kwenye mitaro ya maji barabarani kinyume cha sheria ya mazingira.

Alisema wameanzisha oparesheni ya mtaa kwa mtaa kwa kata 12 zilizopo mjini kwa kushirikiana na maofisa afya wa kata hizo ili kuhakikisha utiririshaji wa majitaka katika mitaro ya barabara unadhibitiwa haraka na kuwachukulia hatua wanaobainika.

"Wakati tunafunga mwaka wa fedha Julai 2020, jumla ya wananchi 120 waliokuwa wametozwa faini ya zaidi ya Sh. milioni 100 kutokana na uchafuzi wa mazingira kutokana na kutozingatia sheria ndogo za Halmashauri ya Mji ya Usafi wa mazingira," alisema Mwebesya.

Aidha, alisema Halmashauri hiyo inazalisha taka ngumu zaidi ya tani 100 kwa siku ambapo kwa sasa wametoa zabuni kwa kampuni mbalimbali za uzoaji taka katika kata 20 ili kuhakikisha mji unakuwa katika hali ya usafi.

# Mgodi wamridhisha Waziri Sima kisa uhifadhi tope sumu

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Musa Sima, ameridhishwa na namna Kampuni ya Shanta Mining inayomiliki mgodi wa dhahabu wa New Luika ulilopo katika kijiji cha Saza, Wilaya ya Songwe, mkoani Songwe kwa ujenzi wa bwawa la kisasa la kuhifadhia tope sumu.

Hali hiyo imeelezwa kwamba itasaidia kutunza mazingira.

Akizungumza baada ya kutembelea mgodi huo, ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya kukagua utunzaji na uzingatiaji wa sheria ya mazingira katika miradi mbali mbali katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Waziri Sima aliipongeza Kampuni ya Shanta kwa kuzingatia maelekezo ya sheria katika ujenzi wa bwawa ili kulinda mazingira. "Bila ujenzi wa bwawa hili kitaalamu sumu zinazozalishwa mgodini zisingedhibitiwa," alisema Waziri Sima.

Aliwataka wawekezaji wengine kujenga miundombinu ya kuhifadhi taka hatarishi na kueleza kuwa madhara ya tope sumu ni makubwa kwa viumbe hai.

Sima ambaye alifuatana na Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC), Prof. Esnati Chaggu, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka pamoja na maofisa wengine wa NEMC, aliwataka watendaji wa halmashauri na ofisa madini wa Wilaya ya Songwe kushirikiana kwa karibu na kuhakikisha wachimbaji wadogo wanatambuliwa katika maeneo yao, wanapewa liseni, ili iwe rahisi kuratibu kukagua shughuli zao na kulinda wa mazingira kwa mujibu wa sheria ya mazingira na kanuni za utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

# RC Malima aifagiliaTBA

**Na Renatha Msungu,** SIMIYU

MKUU wa Mkoa wa Mara, Kigoma Malima, amesema Wakala wa Majengo nchini (TBA), wana uwezo wa kufanya mambo makubwa katika ujenzi, hivyo wanapaswa kuendelea kuboresha kazi yao kwa sababu serikali inawategemea.

Malima aliyasema hayo katika viwanja vya Nyakabindi, mkoani Simiyu wakati alipotembelea banda hilo.

"TBA wanamchango mkubwa katika ujenzi wa nchi hii kwa kujenga majengo yaliyo bora na kwa gharama nafuu," alisema Malima.

Hata hivyo, alisema mchango wa TBA bado unahitajika kwa sababu kuna maeneo mengi yanahitaji ujenzi ili kupendezesha maeneo.

"Kwa mfano hapa Simiyu bado kuna maeneo yanahitaji ujenzi hivyo wao wajipambanue kuhakikisha wanaboresha majengo na kuyajenga," alisema Kigoma.

Pia, alisema TBA bado ina mchango mkubwa katika suala la ujenzi hata wasipopewa majengo lazima waingie kama washauri katika kazi hiyo.

## Askofu asisitiza uwekezaji elimu

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

KANISA la Anglikana Dayosisi ya Mara, limepokea majengo ya vyumba vitatu vya madarasa na ofisi moja ya walimu yaliyojengwa na kampuni ya Mrefu Construction Ltd ya wilayani Bunda, katika Shule ya Msingi Shalom katika halmashauri ya mji wa Bunda mkoani Mara.

Akipokea majengo hayo jana ambayo yamegharimu zaidi ya Sh. milioni 142 pamoja na kodi, Askofu wa kanisa hilo Dayosisi ya Mara, George Okoth, alisema kuwa yamejengwa kwa kiwango kinachotakiwa na kuipongeza kampuni ya Mrefu Construction Ltd, kwa kufanya kazi yake kwa weledi wa hali ya juu na kukamilisha majengo kwa wakati.

"Kwa ujumla kampuni hii ya Mrefu Construction Ltd inafanya kazi nzuri sana na sisi kama kanisa tutakuwa tunaitumia sana kwenye shughuli zetu kwa sababu kiwango kazi nzuri inayoonekana, tena kwa weledi wa hali ya juu," alisema Askofu Okoth.

Askofu Okoth alitumia fursa hiyo kwa kutoa wito kwa wadau wa elimu na taasisi mbalimbali kuwekeza kwenye elimu, kwani elimu ndiyo msingi wa maisha, ili kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu, iliyowekeza kwenye elimu kwa kutoa elimu bila malipo.

Alisema ni wakati sasa wa kuwekeza kwenye elimu kwani ni elimu pekee inayomuondoa mtu kwenye ujinga pamoja na umasikini, na kwamba ndiyo maana Rais John Magufuli amewekeza kwenye elimu kwa kutoa elimu bila malipo.

Kadhalika, alisema kwamba pia kanisa hilo limewekeza kwenye elimu kwa kujenga shule nyingi na vyuo nchini.

Aliongeza kuwa shule hiyo itaendelea kujengwa, na kwamba matarajio yao ni kuwa ya sekondari hapo baadaye na inatoa elimu bora kwa wanafunzi kwa sababu inao walimu wa kutosha na wenye uwezo mzuri wa kufundisha.

Pia Askofu alikemea vitendo vya ukatili wa kijinsia unaofanywa mkoani hapa vikiwamo vya ukeketeji wa mtoto wa kike.

Mkurugenzi wa elimu katika kanisa hilo, Arthur Mauya na mkuu wa shule hiyo, Joyce Barigenge, walisema majengo hayo yako kwenye ubora unaotakiwa.

Mkurugenzi wa kampuni iliyojenga majengo hayo, Kulwa Kahabi, aliwataka makandarasi wenzake kufanya kazi kwa weledi kama Rais Magufuli anavyosisitiza.

# Upatikanaji dawa bado tatizo vituoni

**Na Happy Severine,** BARIADI

SERIKALI imesema bado kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vya umma.

Imeelezwa hali hiyo imesababisha kuendelea kuwapo kwa malalamiko mengi ya wananchi ya kukosa huduma stahiki.

Serikali inabainisha kuwa licha ya bajeti ya afya kuongezeka kwa kiwango kikubwa tangu mwaka 2015 ambayo ilikuwa Sh. bilioni 31 hadi Sh. bilioni 270 mwaka 2019, malalamiko ya wananchi kukosa dawa bado ni mengi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais (TAMISEMI) anayeshughulikia Afya, Dk. Dorothy Gwajima, wakati wa kikao kazi cha watalaamu wa afya Mkoa wa Simiyu pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama.

Dk. Gwajima alisema kuwa licha ya Rais Magufuli kuongeza bajeti Wizara ya Afya kutoka Sh. bilioni 31 mwaka 2015 hadi Sh. bilioni 270, bado malalamiko ya wananchi kukosa dawa yameendelea kutokana na uwapo wa wizi wa dawa na kutotumika ipasavyo kwa mfumo huo.

Naibu Katibu Mkuu huyo alisema Wizara imebaini kuwa tatizo lipo kwenye mfumo na mnyororo wa ugavi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi ambapo watoa huduma hawaufuati ipasavyo.

"Mfumo huu haufuatwi hata kidogo, baadhi ya nyaraka ambazo zinahusika katika uagizaji wa dawa, upokeaji, utunzaji kwenye stoo kubwa na ndogo, pamoja na utoaji wa dawa hazijazwi ipasavyo, na wakati mwingine hawajazi na wakijaza wanafanya vibaya, wakati mwingine hazijulikani dawa wapi zilipo," alisema Dk. Gwajima.

"Tumechunguza kutokana na kutofuata utaratibu wa mfumo huo, kumebainika kuwa kuna wizi mkubwa wa dawa ambao unafanywa na watoa huduma, lakini maeneo mengine dawa zimepokelewa, lakini haijulikani zilipo," alieleza Gwajima.

Kutokana na hali hiyo, alitoa miezi miwili kwa waganga wakuu wa mkoa na wilaya nchini nzima kufanya ukaguzi wa kina wa mfumo na mnyororo wa ugavi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya kama unafanya kazi inavyotakiwa.

Dkt Gwajima aliagiza hadi kufikia Oktoba 15, 2020, taarifa ipelekwe kwake ya ukaguzi huo, huku akitaka kwenye zoezi hilo wajumuishwe wakaguzi wa mahesabu wa ndani, pamoja na kushirikishwa kwa vyombo vya ulinzi na usalama. Awali akitoa taarifa ya mkoa ya ukaguzi wa baadhi ya vituo 22 kati ya 199 vya mkoa mzima, Mganga Mkuu wa mkoa wa Simiyu, Dk. Festo Dugange, alisema dawa zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 70 zimebainika kutumika bila kuonekana kwenye mfumo huo. Alisema katika Hospitali ya Wilaya ya Maswa, walibaini kuwapo kwa upotevu wa dawa zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 50, huku wakibaini katika baadhi ya vituo nyaraka za upokeaji dawa na utuzaji hazijazwi ipasavyo.

Mkuu wa mkoa wa Simiyu, Antony Mtaka, alisema bado kuna changamoto kwenye utendaji kazi wa wafamasia wengi, hali ambayo wananchi wamekuwa wakilalamika kwa kukosa dawa.

Mtaka alisema licha ya serikali kupambana kuongeza bajeti ya dawa, bado wapo watendaji wa afya wamekuwa hawatekelezi majukumu yao ipasavyo na kusababisha malalamiko ya ukosefu wa dawa.

Mkaguzi wa ndani wa mkoa huo, Mika Mollel, alisema baadhi ya mifumo ya ukaguzi wa dawa kwenye Wizara ya Afya haiwapi ruhusa wakaguzi kutekeleza majukumu yao ya ukaguzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.




Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Richard Jordinson (kulia), akikabidhi mkataba wa makubaliano ya Mpango wa Uwajibika kwa Jamii mwaka huu (CSR) kwa Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel (kushoto). **MPIGAPICHA WETU**

# Mkataba wa bil. 9.2/- wa GGML kuinufaisha Geita

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) pamoja na Halmashauri ya Mji wa Geita wamesaini makubaliano ya utekelezaji wa Mpango wa kusaidia Jamii (CSR) kwa mwaka 2020 wenye thamani ya Sh. bilioni 9.2.

Makubaliano hayo yamethibitisha ahadi ya GGML kwa Serikali baada ya kutekeleza mabadiliko yaliyomo kwenye kifungu cha 105 cha Sheria ya Madini ambacho kinajumuisha CSR.

Utekelezaji wa mpango huo wa CSR utanufaisha jamii ya Geita katika maeneo ya mazingira, miundombinu, afya, elimu na biashara ndogo na za kati (SMEs).

Akizungumza katika hafla ya kusaini makubaliano hayo, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel, alielezea namna Serikali inavyothamini ushirikiano mzuri uliopo kati GGML na jamii ya Geita.

Alisema GGML inajitahidi kusaidia Serikali za kuwa na maendeleo endelevu ya jamii na uchumi katika jamii ya mji wa Geita.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Richard Jordinson, alisema hatua hiyo inatekeleza malengo ya kampuni hiyo kuendeleza ushirikiano na serikali za mitaa na jamii nzima kwa ujumla katika kutambua na kusimamia miradi muhimu kwa mustakabali endelevu wa mkoa wa Geita.

"Tunafurahi sana kuendeleza ahadi yetu kwa Serikali na jamii wenyeji.

Katika mwaka huu wa tatu wa utekelezaji wa mpango huu baada ya mabadiliko ya sheria ya madini, ni matumaini yetu kuwa tunaweza kuendeleza tulipoishia katika miradi iliyopita ili kuongeza tija na umiliki kwa jamii lakini pia kuendelea kuahidi ushirikiano katika miradi endelevu ambayo itaendelea kuwepo hata baada ya shughuli za mgodi," alisemas na kuendelea:

"Tangu GGML ianzishwe, imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na serikali ya mkoa wa Geita kusaidia miradi kadhaa ya kijamii katika Mkoa wa Geita kupitia ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi (PPP) sambamba na mpango ya Kitaifa.

"Pamoja na tunu yake kuu ya kusaidia jamii ya Geita kuwa na maendeleo endelevu kijamii na kiuchumi ambayo yatabakia hata baada ya shughuli za uchimbaji kumalizika, pia kampuni imefadhili utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo usambazaji wa majisafi, uendelezaji wa shughuli za uchumi katika sekta za kilimo, ujenzi na huduma."

ama
ALHAMISI AGOSTI 13, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Taasisi ya Chakula & Lishe: tuko juu kunyoyesha vichanga**



Ukurasa 13

Manufaa kamili maziwa ya mama



Ukurasa 12

**Yaliyo muhimu kuzingatiwa kutoka kwa mama anayeendelea kuyonyesha**

AFYA

DURU WIKI YA UNYONYESHAJI

# Waziri Ummy anavyonadi mpango kamili haki ya mtoto kunyonya

**Na Yasmine Protace**

NAMNA isiyo sahihi katika kusaga utumbo wa mtoto, kiafya inaelezwa ni moja ya maeneo ya kupata ugonjwa wa utapiamlo

Ili mtoto awe na afya njema, ni sharti apate mlo sahihi unaomsaidia kukidhi mahitaji ya ukuaji wao na kumlinda dhidi ya maradhi.

Wajawazito ambao wanahudhuria kliniki, wamekuwa wakipatiwa elimu juu ya ulaji vyakula vyenye lishe bora.

Inaelezwa kwamba hata inapotokea wanajifungua, elimu zaidi imekuwa ikiendelea kutolewa kuwasaidia watoto hao kupata chakula bora, ili kiwasaidie katika ukuaji.

Mara zote ni kwamba, msingi wa lishe unapotolewa unamsaidia mtoto namna ya upata kupata lishe bora na ukuaji mzuri.

Inaelezwa, lishe isiyo sahihi inachangiwa na mama kuelemewa na majukumu ya kiuchumi na jamii, pia nyumbani, hivyo wanakosa muda wa kutosha za matunzo, yote ikiishia mtoto kuwa na utapiamlo.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anatamka hayo katika ufunguzi wa Wiki ya Unyonyeshaji, kitaifa aliponadi hayo kwa kauli:

"Ni dhahiri kuwa mchango wa mwanamke katika familia, ajira na uzalishaji kwa ujumla ni mkubwa, hivyo ni muhimu kuwatia moyo na kuwasaidia wanawake ili waweze kufanya majukumu ya uzalishaji na utunzaji familia kwa ukamilifu."



Waziri Ummy Mwalimu, alipoongea na wakazi wa Muheza mkoani Tanga hivi karibuni, katika maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji. **NA MPIGAPICHA WETU**

> **Mara zote ni kwamba, msingi wa lishe unapotolewa unamsaidia mtoto namna ya upata kupata lishe bora na ukuaji mzuri.**

Waziri anasema, jamii ina wajibu wa kuwawezesha wazazi husussani wanawake, wawanyonyeshe watoto wao maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya mwanzo, baada ya kujifungua.

Aidha, anahimiza watoto hao wanapotimiza umri wa miezi sita, waanzishiwe vyakula vya nyongeza vyenye ubora katika mtazamo wa lishe, huku wakiendelea kunyonyeshwa hadi watakapotimiza umri wa miaka miwili.

Kwa upande wa takwimu za hali ya ulishaji watoto nchini Tanzania, takribani asilimia 97 ya watoto wenye umri chini ya miaka miwili, wananyonyeshwa maziwa ya mama.

"Idadi ya watoto wanaoanzishiwa kunyonyeshwa maziwa ya mama kwa wakati sahihi katika kipindi kisichozidi saa moja, baada ya kuzaliwa ni asilimia 53," anasema Waziri Ummy na anaendelea:

"Idadi ya watoto wanaonyonyeshwa maziwa ya mama pekee bila kupewa maji, vinywaji na vyakula vingine katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo baada ya kuzaliwa ni asilimia 58."

Anasema, idadi ya watoto wanaoanzishiwa vyakula vya nyongeza kwa wakati sahihi katika umri wa miezi sita hadi nane, ni asilimia 87 na idadi ya watoto wenye umri wa miezi sita hadi 6 23, wanaolishwa chakula kinachokidhi vigezo vya ubora kilishe, ni asilimia 35.

"Vigezo hivyo, ni idadi sahihi ya milo anayopewa mtoto kwa siku, kulingana na umri wake na mlo uwe na mchanganyiko wa vyakula kutoka kwenye makundi yasiyopungua manne ya vyakula.

Anasema Maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani kwa Mwaka 2020, yamebebwa na kaulimbiu: 'Tuwawezeshe Wanawake Kunyonyesha Watoto kwa Afya Bora na Ulinzi wa Mazingira."

Anaitaja kuwa ni kaulimbiu inayolenga kukumbusha mchango wa unyonyeshaji katika utunzaji mazingira na ikolojia duniani, sanjari na kulinda afya ya binadamu.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, ni kaulimbiu inayohimiza jamii kuboresha kasi ya unyonyeshaji, sanjari na kupunguza kiwango cha utumiaji maziwa na vyakula mbadala vya watoto wachanga na wadogo.

"Tukumbuke kuwa, matumizi ya maziwa na vyakula mbadala vya watoto wachanga na wadogo, yanakwenda sanjari na matumizi ya vifungashio mbalimbali, vikiwamo vya plastiki, nishati ikiwemo kuni na mkaa, maji, chupa za kulishia watoto na ongezeko la hewa ya ukaa inayoathiri mazingira ya dunia," anahitimisha.

AFYA

DURU WIKI YA UNYONYESHAJI

# Yaliyo muhimu kuzingatiwa kutoka kwa mama anayeendelea kuyonyesha

**Na Mwandishi Wetu**

KUMNYOYESHA mtoto maziwa ya mama, inaelekezwa itekelezwe ndani ya saa moja baada ya kujifungua, apate maziwa ya mwanzo yenye rangi ya njano (Colostrum), yanayomsaidia kutoa kinyesi cha mwanzo kwa urahisi na kumpunguzia maumivu ya tumbo, akipata kinga nyingi ya athari mwilini.

Ni huduma anayoipata miezi sita bila kumpa kingine chochote, ikiwamo maji ya kunywa.



Watoto wachanga wakifaidi maziwa ya mama kwa stadi stahiki inayoshauriwa na wataalamu wa afya. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### INAWEZEKANAJE?

Mama anatakiwa kumuweka vizuri mtoto kwenye chuchu wakati wa kumnyonyesha, kwa kuhakikisha sehemu ya eneo jeusi linalozunguka chuchu ya mama, linakuwa limeingia mdomoni mwa mtoto aliyeweka kinywa vizuri kwenye titi.

Pia, mama anapaswa kuhakikisha mkono mmoja unamshika mtoto kuanzia makalioni kwake na kichwa chake kilale kwenye kiwiko cha mkono huo.

Kingine, mkono unapaswa ushike titi analonyonya mtoto, huku kidole gumba kikiwa juu na vidole vinne vilivyobaki vinakaa chini ya chuchu.

Mtoto anyonye titi moja kwa muda mpaka liishe kabisa, ndio ahamishiwe jingine, ili apate maziwa ya mwanzo yenye maji kwa kiasi kikubwa na maziwa ya mwisho mazito yenye mafuta kwa wingi.

Kumnyonyesha mtoto kila mara anapohitaji ikiwamo usiku. Viashiria vya mtoto kuhitaji kunyonya vinajionyesha katika kilio na kujilamba, akiwa ameshapata haja mara kadhaa au alilala kwa muda kidogo zaidi ya saa mbili.

Mama aweke mawazo yote kwa mtoto na kumwangalia kwa upendo wakati wa unyonyeshaji, kusaidia maziwa kuzalishwa kwa wingi

Ni muhimu mama aepuke msongo wa mawazo, kwani unaathiri uzalishaji maziwa, pia apate muda wa kupumzika

Jambo muhimu linasisitizwa ni kwamba mama amuweke mtoto begani kwa muda kidogo kila anapomaliza kumnyonyesha, ili atoe gesi tumboni kwa njia ya kubeua

Mama huyo asisahau binafsi kupata mlo kamili wa kila siku, ili amudu kuzalisha maziwa ya kutosha.

### MLO WA MZAZI

Protini; hapo kuna vyakula vya jamii ya nyama, samaki, dagaa, maziwa, mayai, jibini, maini, figo, senene, nzige, kumbikumbi na wadudu wanaoliwa, maharage, njegere, kunde, njugumawe, choroko na dengu.

Faida yake ni kukarabati sehemu za mwili zilizochakaa ili kuimarisha kinga, kuzuia upungufu wa damu na kuuwezesha mwili kufanya kazi kwa ufanisi.

Wanga; inajumuisha nafaka, mizizi na ndizi. Ndivyo vitu navyochukua sehemu kubwa ya mlo na kwa kawaida ndiyo vyakula vikuu, vikiwa na jukumu la kuupa mwili nguvu ya kufanya kazi.

> **“Iwapo mama atalazimika kwenda kazini au kumuacha mtoto nyumbani kwa sababu yoyote ile, anaweza kukamua maziwa yatakayomfaa mtoto wakati hayupo.**



Hapo kuna mahindi, mchele, mtama, ulezi, ngano, uwele, muhogo, magimbi, ndizi na jamii ya viazi vikuu, vitamu na mviringo.

Vitamini na Madini; mjumuiko wake unabeba matunda aina zote, kama papai, embe, pera, limau, pesheni, nanasi, peasi, chungwa, chenza, zambarau, parachichi, ndizi mbivu, fenesi, stafeli, mabungo, madalansi na topetope.

Aidha, kuna matunda pori kama ubuyu, ukwaju na na embe ng'ongo. Juma yao yote, zinaupa mwili uwezo wa kuzuia na kupambana na maradhi, pia kuuwezesha mwili kufanya kazi kwa ufanisi na kulainisha choo

Mboga: Ni kundi linalojumuisha aina zote za mboga zinazolimwa na asilia, katika orodha yake zimo mchicha, kisamvu, majani ya kunde, matembele, spinachi, mnafu na mchunga.

Aina ni karoti, pilipili hoho, biliinganya, matango, maboga, nyanya chungu, bamia, na kabichi, zikiwa na manufaa ya kuupa mwili uwezo wa kuzuia na kupambana na maradhi, kulainisha choo na kuuwezesha mwili kufanya kazi kwa ufanisi.

### VYAKULA MAFUTA

Inatajwa kuwa muhimu, ila ni kiasi kidogo ndicho kinachohitajika mwilini. Yanaweza kutoka mimea kama mbegu ya alizeti, ufuta, pamba, korosho, karanga na mawese.

Pia, mafuta yanapatikana kutoka kwa wanyama, mfano hai ni siagi, samli, nyama iliyonona na baadhi ya samaki, zikiwa na mchango wa kuupa nguvu kwa kiasi kikubwa.

Maji yanapaswa kutumika yaliyo safi na salama, walau lita moja na nusu (glasi nane) kwa siku, ili kuzuia kusaidia maziwa kuzalishwa kwa wingi.

Vilevile, mtu anaweza kuongeza maji mwilini kwa kunywa supu, madafu, togwa na juisi halisi za matunda mbalimbali.

Manufa haya moja kwa moja, ni maziwa kutoka kwa wingi na kuzuia upungufu wa maji mwilini.

### UKAMUAJI MAZIWA

Mama anaweza kukamua maziwa yake kwa kutumia mkono au kifaa maalum ya kukamulia (breast pump) na uhifadhi.

Iwapo mama atalazimika kwenda kazini au kumuacha mtoto nyumbani kwa sababu yoyote ile, anaweza kukamua maziwa yatakayomfaa mtoto wakati hayupo.

Hatua ya kwanza, ni mama ananawa mikono au kuoga vizuri na kisha anasafisha chombo cha kukamulia.

Kamata ziwa kwa vidole vyako na dole gumba likiwa pembeni mwa eneo jeusi linalozunguka chuchu. Kandamizia ziwa kwenye kifua chako, halafu bonyeza vidole pamoja kulekea kwenye chuchu.

### USALAMA WAKE

Maziwa yanadumu kati ya saa sita hadi nane kwenye joto la kawaid ana inapowekwa kwenye jokofu sehemu ya kawaida inadumu saa 24 na sehemu ya kugandisha inakaa kwa saa 72.

Mtu anapoyatoa kwenye jokofu, ahakikishe kabla ya kumnywesha mtoto yawe na joto la vuguvugu, kifaa cha kumywesha ni kikombe kisafi kilicho na joto wakati wa kutumika.

Mama anashauriwa kuepuka kutumia chupa za chuchu, kwani si rahisi kusafisha na huhifadhi uchafu, vivyo hivyo, anapaswa kuzingatia usafi wa mwili wake na vyombo wakati wa kukamua maziwa, ili kumuepusha mtoto na uchafu kupitia maziwa anayotumia (contamination)

### MWENYE VVU

Kuna cha kujiuliza, je, ni salama kunyonyesha iwapo mama ana Virusi vya Ukimwi (VVU)? Hapo kuna jibu kwamba, dawa za kufubaza VVU zikitumiwa na mama na mtoto, zinazuia watoto wachanga kupata maambukizi wakati wa unyonyeshaji.

Mtoto anatakiwa apewe dawa hizo kila siku, angalau kwa wiki sita na kama mama hakupata dawa za VVU kwa kipindi chote cha ujauzito na mtoto anapaswa apewe angalau kwa wiki 12.

Kama mama hatumii dawa za VVU, mpe mtoto dawa hadi wiki moja baada ya kuachishwa ziwa.

AFYA

DURU WIKI YA UNYONYESHAJI

# Manufaa kamili maziwa ya mama

**Na Mohammed Sharksy,** UNGUJA

KUTOKANA na utandawazi uliko, hivi sasa kuna baadhi ya kinamama wanaoelezwa hawanyonyeshi watoto wao ipasavyo, hasa walioko umri kati ya miaka 20 na 35, wakiwa na hofu kuwa maziwa yao 'yataanguka' na kuwapotezea mvuto wa haiba ya kike.

Hilo linatokea, huku kunyonyesha kukiwa sehemu muhimu inayomuunganisha mama na mwanawe, hivyo mtoto anapokoseshwa mlo huo, ina maana kunapoteza ukaribu wa uhusiano.

Kimsingi, kunyonyesha ni kitendo mama mzazi anampa mtoto wake maziwa kutoka matiti yake moja kwa moja au kumnywesha maziwa yaliyokamuliwa kwa kutumia kikombe.

Maziwa ya mama ni chakula na kinywaji cha kwanza na cha pekee kwa mtoto mara anapozaliwa mpaka kufikia umri wa miezi sita, pasipo mlo mbadala ikiwamo maji ya kunywa.

Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF), vyote vinapendekeza mtoto aanze kunyonya maziwa ya mama saa moja baada ya kuzaliwa.

Maziwa yanajulikana kwa ubora wake kwa mtoto mchanga, kuliko mbadala wowote, yakiwapatia virutubisho vyote stahiki katika miezi ya mwanzo maishani.

Kwa kurejea maelekezo ya WHO, mtoto afikishapo umri miezi sita, ndipo anapopaswa kupewa vyakula vya nyongeza, huku akiendelea kunyonyeshwa maziwa ya mama hadi kufikia miaka miwili.

Kwa maana hiyo, ziko faida nyingi anazopata mtoto, mama na baba kwa jumla.



Kinamama wakiendelea kunyoyesha watoto wao. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### ANAVYOFAIDI MTOTO

Mtoto anaponyonyeshwa saa moja baada ya kuzaliwa ananufaika na kinga ha kwanusuru na vifo.

Virutubisho vinavyopatikana kwenye maziwa ya mama, mchangayiko wake ni wa kimaumbile zaidi, kwa sababu yanatolewa kiasili zaidi na hayana gharama.

Lingine analolitaja ni manufaa ya kisaikolojia yanayosaidia kujenga uhusiano mzuri kati ya mama na mtoto mchanga.

Maziwa kutoka titi la mama, linaelezwa kumpatia mtoto vyakula vyote sita muhimu na virutubisho vinavyomjengea mtoto mwili, katika uwiano sahihi katika ukuaji na maendeleo ya mwili. Hapo kuna jamii ya protini, vitamini, wanga, sukari, maji, na madini,

Unyonyeshaji bora wa maziwa ya mama, pia unatajwa kujenga uhusiano wa karibu kati ya mama na mtoto anayepatiwa kinga dhidi ya maradhi kama kuharisha, magonjwa ya njia ya hewa na masikio.

Manufaa mengine ya maziwa ya mama, ni kwamba humuwezesha mtoto kukua kimwili na kiakili katika ukamilifu unaostahili, huku uhusiano kati ya mama na mtoto hufikia ngazi bora.

Mara zote mtoto anayenyonya maziwa ya mama huwa na mwenendo mzuri kiakili, akilinganishwa na asinyenyonya.

Kunyonyesha mtoto kunasaidia kumkinga na magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na yasiyoambukiza, kwani anawekwa salama na mwenye joto la kutosha akiwa pembeni mwa mama yake.

Mtoto huyo ananufaika na maziwa ya mama, hata kiakili anakuwa katika uwezo bora katika utambuzi, mahudhurio shuleni na hatimaye kufikia maisha bora katika utu uzima

Maziwa ya mama yanatoa kinga inayodumu muda mrefu dhidi ya magonjwa kama kisukari, mzio na saratani mbalimbali katika maisha ya mtoto.

> **Maziwa ya mama yanatoa kinga inayodumu muda mrefu dhidi ya magonjwa kama kisukari, mzio na saratani mbalimbali katika maisha ya mtoto.**



### MAMA ANUFAIKA

Maziwa ya mama huchangia kulinda afya ya mtoto kwa njia mbalimbali, ikiwamo baada ya mama kujifungua, inasaidia tumbo la uzazi kurudi katika hali ya kawaida mapema na kupunguza damu kutoka.

Maziwa ya mama yanapunguza uwezekano wa kupata ujauzito katika miezi sita ya mwanzo kama mama atamnyonyesha mtoto maziwa yake mara nyingi kwa siku

Ni maziwa hayo yanapunguza uwezekano wa mama kupata saratani za matiti na mfuko wa uzazi, huku kukiwapo uhusiano wa karibu kati ya mama na mtoto.

Iwapo mama aliongezeka uzito wakati wa mimba, kunyonyesha kunamsaidia kurudia umbile lake la kawaida, akijengeka kiafya, kisaikolojia na mapenzi hali ya juu.

### ANAVYOFAIDI BABA

Kiuchumi, kunatajwa maziwa ya mama gharama yake ni nafuu na hakuna haja ya kununua vyakula na vifaa mbadala.

Aidha, kwa vile maziwa ya mama ni kinga tosha kwa mtoto, inampunguzia baba gharama za matibabu ya mtoto na anapata muda wa kutosha kujikita katika nyingine muhimu kifamilia kama vile chakula na, huduma za masomo kwa wanafunzi.

### KITAIFA

watoto wanapotunzwa vizuri, kuna mchango katika kupunguza gharama za matibabu na hasa kwa wale wenye umri chini ya wa miaka mitano, kutokana na afya njema walionayo.

Mwongozo mkuu kwa mtoto ni anapaswa kuendelea kunyonya maziwa ya mama mpaka anapofikisha umri miaka miwili.

*Mwandishi wa makala hii ni Mkufunzi Msaidizi katika Shule ya Afya Sayansi za Tiba, katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, mawasiliano yake ni simu: (+255) 0777 432 493 na barua pepe: mohammed.rashid96@yahoo.com.*

AFYA

DURU WIKI YA UNYONYESHAJI

# Taasisi ya Chakula & Lishe: tuko juu katika kunyoyesha vichanga



Maisha ya urafiki wa mama na mtoto, katika duru ya kunyonya na kunyoyesha. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mary Geofrey**

KATI ya Agosti Mosi hadi 7 ya kila mwaka, Tanzania huungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha wiki ya unyonyeshaji maziwa ya mama.

Inaelezwa kuwa fursa ya kipekee inayounganisha wadau mbalimbali kufikia malengo ya azimio lililopitishwa mwaka 1990, linalosisitiza umuhimu wa kulinda, kuimarisha na kuendeleza unyonyeshaji maziwa ya mama, lengo ni kuwawezesha wanawake wanyonyeshe kwa kufuata taratibu sahihi.

Mkurugenzi wa Elimu na Mafunzo ya Lishe wa Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) Sikitu Kihinga, anaelezea umuhimu wa maadhimisho hayo nchini, kwamba mbali na wajibu wa mama mazazi kumnyonyesha mtoto maziwa saa moja baada ya kujifungua, pia ana wajibu wa kumnyonyesha mtoto kila mara usiku na mchana.

Anasema hilo linafanyika kadri wajibu unavyojitokeza, huku akimtaka mama ajipangie ratiba maalum, mtoto akinyonyeshwa maziwa ya mama kwa miezi sita mfululizo, pasipo mlo mwingine wowote, ikiwamo maji .

Sikitu anasema katika maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji duniani mwaka huu, kaulimbiu yake "'Tuwawezeshe wanawake kunyonyesha watoto kwa afya bora na ulinzi wa mazingira.'

Anafafanua ujumbe huo kwa kauli: "Inalenga kutukumbusha mchango wa unyonyeshaji katika utunzaji wa mazingira ya dunia na ikolokia yake sanjari na kulinda afya ya binadamu."

Ofisa huyo wa TFNC, anasisitiza kaulimbiu hiyo inahimiza jamii kuboresha kasi ya unyonyeshaji, sanjari na kupunguza kiwango cha matumizi ya maziwa na vyakula mbadala vya watoto wachanga na wadogo.

> “ Vigezo hivyo ni idadi sahihi ya milo anayopewa mtoto kwa siku kulingana na umri wake na mlo uwe na mchanganyiko wa vyakula kutoka kwenye makundi yasiyopungua manne ya vyakula.



Aidha, anakumbusha matumizi ya maziwa na vyakula mbadala vya watoto wachanga, yanaenda sanjari na suala la umakini na matumizi ya vifungashio mbalimbali vikiwamo vya plastiki na nishati ya kuni na mkaa, maji, chupa za kulishia watoto, akioanisha na ongezeko la hewa ya ukaa inayoathiri mazingira ya dunia.

**MALENGO TFNC**

Sikitu anasema anaorodhesha malengo ya maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji maziwa ya mama kwa mwaka huu, ni kuihamasisha jamii iendeleze juhudi za kulinda, kuhimiza na kudumisha nyonyeshaji watoto maziwa ya mama, kama njia mojawapo ya kutunza mazingira na kukabili athari za mabadiliko ya tabia za nchi.

Anasema, pia kuna suala la kuimarisha fikra za jamii iwajibike kulinda, ihimize na kuendeleza unyonyeshaji watoto maziwa ya mama, ikiwa ni uamuzi sahihi wa kutunza mazingira na kukabiliana na athari za na mabadiliko ya tabia nchi.

Sikitu analitaja lingine ni kuishirikisha jamii katika juhudi za kulinda, kuhimiza na kuendeleza unyonyeshaji watoto maziwa ya mama, ili kufuikia kupatikna matokeo chanya.

Lingine ni kuhamasisha jamii ushiriki katika mikakati ya kuboresha afya kupitia kulinda, kuhimiza na kuendeleza unyonyeshaji watoto maziwa ya mama.

**ILIVYO NCHINI**

Ofisa huyu wa asasi msimamizi wa Chakula na Lishe nchini, anasema takwimu za hali ya ulishaji watoto nchini zinaonyesha takribani asilimia 97 wenye umri chini ya miaka miwili wananyonyeshwa maziwa ya mama.

Pia, wanaonyonyeshwa maziwa ya mama pekee bila kupewa maji, vinywaji na vyakula vingine katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo baada ya kuzaliwa ni asilimia 58.

"Ninaamini kuwa katika kipindi hiki cha maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji duniani, jamii itakumbushwa wajibu wao mkubwa katika kuwezesha wazazi kufanikisha unyonyeshaji ili kuboresha zaidi hali ya lishe ya watoto," anasema Sikitu.

Anasema pia idadi ya watoto wanaonzishiwa vyakula vya nyongeza kwa wakati sahihi katika umri wa miezi sita hadi nane ni asilimia 87.

Lingine, ni kwamba idadi ya watoto wenye umri wa miezi sita hadi 23 wanaolishwa chakula kinachokidhi vigezo vya ubora wa lishe ni asilimia 35.

"Vigezo hivyo ni idadi sahihi ya milo anayopewa mtoto kwa siku kulingana na umri wake na mlo uwe na mchanganyiko wa vyakula kutoka kwenye makundi yasiyopungua manne ya vyakula," anasema.

**FAIDA ZA UNYONYESHAJI**

Sikitu anafurahia lishe sahihi na hususan kunyonyesha maziwa ya mama, kwamba kuna faida zinazoboresha hali ya lishe, ukuaji na maeneo yao kimwili na kiakili kwa watoto nchini.

Anasema, kunasaidia kupunguza kasi ya magonjwa hatari ya kuambukizwa na vifo vya watoto nchini na kinamama wanaonyonyesha wanakuwa mbali na uwezekano wa kupata maambukizi kama saratani ya matiti na athari za ki uzazi.

Sikitu anaeleza kuwapo faraja ya kuongezeka imani miongoni mwa jamii na wanawake kuwa unyonyeshaji ni njia bora zaidi na asili ya uzalishaji watoto.



# NFRA yataja mafanikio 10 miaka mitano

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), imetaja mafanikio 10 yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka mitano ikiwamo kuongezeka kwa uhifadhi wa nafaka kutoka tani 251,000 hadi tani 501,000.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala huo, Milton Lupa, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utendaji wa NFRA kwa miaka mitano.

Alisema kuongezeka kwa uwezo huo kumechangiwa na mradi wa ujenzi wa vihenge 56 na maghala tisa ya kisasa ambavyo kwa pamoja kumeongeza uwezo wa kuhifadhi tani 250,000.

"Kwa sasa mradi huu umefikia asilimia 75 ya utekelezaji na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2020/21. Maghala yana uwezo wa kuhifadhi kwa takriban miaka mitatu tu kabla ya kuanza kupoteza ubora lakini kwa kutumia vihenge vya kisasa, akiba itahifadhiwa zaidi ya miaka mitano bila kupoteza kiwango cha ubora," alisema.

Aidha, alisema kwa kipindi hicho, wakala imehakikisha usalama wa chakula kwa kuhifadhi akiba ya kutosha kila mwaka na kutoa au kuuza akiba ya chakula kwa ajili ya kukabiliana na majanga mbalimbali.

"Wakala imeuza akiba ya chakula ndani ya nchi katika halmashauri za wilaya mbalimbali zilizokabiliwa na upungufu wa chakula, hivyo kupata fedha za kununulia akiba mpya ya chakula," alisema.

Pia alisema wakala imeingiza fedha za kigeni kwa kuuza nafaka nje ya nchi ikiwamo Zimbabwe na kuuza nafaka kwa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) ambalo hupeleka chakula hicho katika nchi mbalimbali ndani ya Afrika.

"Wakala imetoa msaada wa chakula kwa nchi za Malawi na Sudani ya Kusini zilipokumbwa na janga la mafuriko na upungufu wa chakula,"alisema.

Kuhusu kuchangia uchumi, alisema NFRA imekuwa ikinunua nafaka kutoka kwa wakulima na vikundi vya wakulima kila mwaka kwa bei nzuri, hivyo kuchangia kuboresha maisha ya wakulima kutokana na mapato yatokanayo na mauzo ya nafaka.

Kadhalika, alisema kupitia ununuzi wa nafaka, NFRA imekuwa ikichangia mapato ya halmashauri zinazohusika katika ununuzi wa nafaka kwa kulipa ushuru wa mazao. Akizungumzia utoaji wa ajira, Lupa alisema wakala imechangia katika kutoa fursa za ajira wakati wa ununuzi wa nafaka na utekelezaji wa mradi wa kuongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka ambapo takriban wananchi 7,000 wameajiriwa.

Ofisa huyo alisema wakala kila mwaka hushirikiana na vikundi mbalimbali vya wakulima na vyama vya ushirika kununua nafaka kutoka ushirika na kutoa mafunzo ya uhifadhi wa nafaka.

"Pia Wakala umekuwa ukishirikiana na sekta binafsi katika kutekeleza majukumu yake kwa kununua huduma na bidhaa mbalimbali zikiwamo vifaa vya uhifadhi, usafirishaji wa nafaka na bidhaa na huduma kuchangia katika kuwaongezea kipato," alisema.

Lupa alisema mkakati wa wakala ni kupanua wigo wa uhifadhi na masoko ili kuhifadhi chakula cha kutosha na kupata masoko zaidi ya nafaka ndani na nje ya nchi.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene (mwenye suti), akikagua shamba la mboga la Jeshi la Magereza, katika eneo la Nzuguni jijini Dodoma jana, alipotembelea kujionea shughuli mbalimbali za uzalishaji mali za jeshi hilo. **PICHA PAUL MABEJA**

# TFS kupambana na uzalishaji bangi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), imesema itahakikisha hakuna misitu itakayotumika kuzalisha, kusafirisha na kuhifadhi dawa za kulevya ikiwamo bangi.

Akifungua jana mafunzo kwa wahifadhi misitu nchini, Kamishna wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alisema TFS ina wajibu wa kuhakikisha ulinzi na usalama wa nchi hasa kuzuia matumizi ya dawa za kulevya kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama .

"TFS inaandaa mpango mkakati wa vihatarishi katika misitu, hivyo baada ya mafunzo haya tutaweka kipengele cha kupambana na dawa za kulevya. Lengo ni kuhakikisha misitu yetu inabaki kuwa salama na kivutio kwa maeneo ya mipakani," alisema Prof. Silayo.

Aliwaagiza watumishi wa wakala kuwajibika na kujitoa zaidi katika mapambano hayo na kutoa taarifa kwa Mamlaka husika mara wanapobaini uwepo viashiria vyovyote kuhusu dawa za kulevya katika maeneo yao.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Kamishna Mkuu wa Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya nchini, James Kaji, alisema wataendelea kupambana bila woga ili kutokomeza biashara hiyo.

Kaji aliwataka Watanzania kushiriki katika mapambano hayo kwa kutoa taarifa kwa mamlaka kila wanapoona kuna viashiria vyovyote.

Alitaja bangi bado ni tatizo linalowasumbua kutokana na kulimwa katika misitu mikubwa nchini ambayo si rahisi kuyafikia maeneo hayo kama utakosekana ushirikiano na TFS.

Kadhalika, aliwataka wanasiasa kuacha mapendekezo ya kutaka bangi ihalalishwe kwa kuwa madhara ya madawa hayo ni makubwa kuliko faida.

# Mavunde awapa somo vijana kuhusu uchaguzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, amewataka vijana kushiriki katika uchaguzi mkuu na kutumia haki yao kikatiba katika hali ya amani na utulivu.

Mavunde alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akitoa tamko la serikali la Siku ya Vijana Duniani.

"Lazima tutambue umuhimu huu wa uchaguzi kwa kuwawezesha vijana wetu kwenda kupiga kura kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa. Hii ni haki yao kikatiba na kamwe wasitumiwe vinginevyo," alisema.

Aliwataka kutambua kuwa hakuna taifa lolote duniani lenye maendeleo bila amani kwa kuwa ni nguzo kubwa ya umoja na demokrasia ya kweli nchini.

Pia alisema serikali ya awamu ya tano imetoa fursa kwa vijana na kuchangia kuwepo na mwamko mkubwa wa wao kushiriki kwenye siasa za uongozi.

"Mwaka huu umekuwa mwaka wa kipekee ambao umeleta mwamko wa vijana kugombea na asilimia 90 waliojitokeza ni vijana, wamebadilika na hawakai tena nyuma, wapo mbele katika kulijenga taifa lao," alisema.

Akizungumzia kuhusu siku hiyo, Mavunde alisema Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani ya mwaka 2020 inaeleza kuwa idadi ya vijana ni bilioni 1.8 ambayo ni sawa na asilimia 24 ya watu wote ambao ni bilioni 7.5.

Hata hivyo, alisema Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inakadiria kuwa ifikapo mwaka 2035, idadi ya vijana itafikia asilimia 34.5 ambayo ni sawa na watu milioni 19.9 ya Watanzania milioni 57.6.

Kwa upande wa nguvu kazi, Mavunde alisema Shirika la Kazi Duniani (ILO) linabainisha kuwa uelekeo wa nguvu kazi duniani mwaka 2020, asilimia 41.2 inatokana na vijana huku Tanzania nguvu kazi asilimia 56 ni vijana.

Alitaja mambo mbalimbali yaliyofanyika nchini kwa ajili ya vijana ikiwemo programu ya kukuza ujuzi wa nguvu kazi ambapo vijana 28,941 wamepatiwa mafunzo ya uanagenzi kwa fani za ufundi stadi wa ushonaji nguo, useremala, uashi, uchongaji vipuri, umeme, upishi na huduma za hoteli.

Pia alisema serikali imeanzisha programu ya stadi za maisha kwa vijana walio nje ya shule kwa lengo la kuhakikisha kuwa vijana wanakabiliana na changamoto zitokanazo na shinikizo rika.





# CHADEMA yatamba kuendelea kuendeleza uongozi Jiji Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWENYEKITI wa Baraza la Vijana wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo Chadema (BAVICHA), Jimbo la Mbeya Mjini, Steven Jonas ambaye pia ni Kaimu Mwenyekiti wa Chama hicho Mbeya Mjini, amesema chama kimejiandaa kwa namna yeyote ile kuhakikisha jimbo litaendelea kuwa chini ya chama hicho.

Jonas aliyasema hayo jana kwenye ofisi za Chama hicho iliyopo Kata ya Sinde, ambapo alidai kuwa wamejipanga kuendelea kutawala Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa kuhakikisha wanashinda kata zote 36. Alisema ujasiri huo unatokana na wananchi kuendelea kuwaunga mkono kupitia jitihada mbalimbali wanazofanya za kuwaletea maendeleo.

"Kama chama tawala Mbeya mjini, tutaendelea kutawala jiji endapo uchaguzi utakuwa huru na haki kwa kufuata kanuni na sheria, hatutakubali kuona tunafanyiwa uhuni na wasimamizi wa uchaguzi na ikitokea tutapambana nao kufa kupona, lakini hata CCM akishinda kwa haki tuko tayari kumuunga mkono," alisema Jonas. Katika hatua nyingine, Jonas aliwahakikisha wana-CHADEMA wote ambao waliingia kwenye kiny'ang'anyiro cha kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kuendelea kuwa watulivu wakati kamati kuu ikiendelea na mchakato wa mgombea ambaye atakiwakilisha vyema chama kwenye uchaguzi.

Alisema chama kimeshatoa majina ya wagombea wa uchaguzi wa madiwani kwa kata zote 26 za Jimbo la Mbeya Mjini, na kwamba chama pia kimefanya mabadiliko ya wagombea mbali na ambao waliongoza kwenye kura za maoni, lengo likiwa ni kumtafuta mtu sahihi ambaye ataleta ushindani mkubwa kwenye uchaguzi.

Awali Mwenyekiti wa Chama hicho ambaye ni mgombea ubunge jimbo la Mbeya Vijijini, Joseph Mwasote, aliwahakikishia wananchi mkoani Mbeya kuwa watapata ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu ujao kwa sababu ya mambo mazuri waliyoyafanya. Alisema CHADEMA ni chama kikubwa cha upinzani ambacho sera za taratibu zake ni shirikishi, hivyo kitaendelea kupata ushindi kwenye nafasi ya udiwani na ubunge.



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Sima (wa pili kulia), akipata maelezo kwa Meneja wa kiwanda cha bia cha TBL, mkoani Mbeya, Emanuel Sawe (wa pili kushoto), kuhusu baadhi ya mitambo ya uzalishaji alipotembelea kiwanda hicho, mkoani humo, jana. Wengine ni maofisa wa Serikali wa kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utafiti wa mbegu bora ya alizeti watakiwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Nchini (TARI), Kituo cha Uyole, imetakiwa kufanya utafiti wa kina kutafuta mbegu bora za zao la alizeti itakayowasaidia wakulima kupata mazao mengi.

Wito huo ulitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, wakati akizungumza na Nipashe, baada ya kumalizika kwa maonyesho ya wakulima (Nanenane).

Alisema ni wakati sasa kwa Taasisi hiyo kituo cha Uyole kuwasaidia wakulima wa zao hilo kwa kuwapatia mbegu bora ambazo zitasaidia kupata mavuno mengi.

Alisema kwa sasa wakulima wengi wa zao la alizeti wanalima mashamba makubwa na kuyahudumia kwa kufuata kanuni za kilimo bora, lakini wakati wa mavuno wanaambulia mazao machache yasiyolingana na nguvu au rasilimali walizozitumia.

"Mimi naona hapa tatizo ni aina ya mbegu wanazopanda wakulima ndizo zinasababisha wapate mazao kidogo, hivyo nawataka watafiti wa kilimo kupitia kituo chetu cha Uyole, fanyieni kazi suala hili kwa kutafuta mbegu nzuri zitakazoondoa tatizo hili kwa wakulima wetu," alisema Ntinika.

Alisema zinahitajika mbegu ambazo zitamfanya mkulima afaidi jasho lake kwa kupata mavuno mengi ili aweze kurejesha gharama alizotumia na kuambulia faida inayokidhi mahitaji yake.

Awali wakulima wadogo wa alizeti walisema wanalima zao la alizeti kwa kufuata ushauri wa wataalamu wa kilimo na wamekuwa wakijitahidi kupanua mashamba yao ili wapate mavuno ya kutosha, lakini jitihada hizo zimekuwa haziwasaidii kujikwamua na umasikini.

Salehe Mwasole, mmoja wa wakulima wa alizeti wilayani Mbeya, alisema kuwa kulima alizeti kunahitaji moyo kwa vile mkulima anaweza kulima shamba kubwa kwa gharama za juu, lakini mavuno yanapatikana kidogo ambayo hayalingani na gharama za uzalishaji.

Alisema kuwa kitendo hicho kinawakatisha tamaa kuendelea kulima alizeti, na baadhi ya wakulima wameamua kulima mazao mengine kama vile mahindi ambayo angalao yanawapatia faida kidogo. "Tunalima alizeti kwa gharama kubwa, lakini mavuno hayalingani na ukubwa wa mashamba tunayolima wala gharama tunazotumia, ukipata hasara mwaka huu hutamani tena kurudia labda uwe na moyo mugumu, ndio sababu wapo wakulima wenzetu wamekata tamaa na kuamua kulima mazao mengine," alisema Mwasole.

Kwa upande wao, baadhi ya wawekezaji wa viwanda vidogo vya kukamua mafuta ya alizeti, walisema kuwa tatizo walilonalo ni ukosefu wa malighafi ya kukidhi mahitaji ya viwanda vyao.

James Mwailonga, ambaye anamiliki kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti jijini Mbeya, alisema viwanda vingi vya kukamua mafuta ya alizeti vinafanya kazi kwa muda mfupi hasa wakati wa mavuno na baada ya hapo hufungwa kutokana na ukosefu wa malighafi.

## Mtaalamu ataka bajeti iandaliwe kuanzia familia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JAMII imetakiwa kuzingatia upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia ili iweze kuibua miradi mbalimbali inayolenga kuwaletea maendeleo na kusaidia kutatua matatizo yanayowakabili.

Mtaalamu mwelekezi wa masuala ya bajeti ambaye pia ni Mkurugenzi wa Shirika la (Elimisha), Festo Sikagonamo, aliyasema hayo jana wakati wa mafunzo ya upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia kwa vijana wa Kanisa la Calvary Assembles of God (CAG) njia panda lililopo Kata ya Igawilo jijini Mbeya. Sikagonamo alisema iwapo watu watapanga bajeti kwa kuzingatia mahitaji muhimu, itasaidia watu kujitegemea, kuibua miradi yenye kuleta matokea chanya, kupunguza ombaomba pamoja na kupunguza idadi ya watu wasiokuwa na kazi.

Aidha, alisema elimu hii inatolewa kwa makundi yote wakiwamo wanawake, vijana na watu wazima wanaojishughulisha na shughuli za ujasiriamali, kilimo, wafanyakazi na shughuli nyingine.

"Suala la upangaji bajeti kuanzia ngazi ya familia ni muhimu sana, hivyo Shirika la Elimisha lilianzisha programu hiyo kwa lengo la kuwasaidia wananchi kuheshimu matumizi ya rasilimali wanazozipata kwa lengo la kujitegemea," alisema Sikagonamo.

Akizungumza na Nipashe baada ya mafunzo hayo, Daudi Mbongo ambaye ni mlezi wa vijana katika kanisa la CAG, alisema waliamua kutoa mafunzo hayo kwa vijana baada ya kuona vijana wengi hawana shughuli maalumu za kuwaingizia kipato.

Vijana walioshiriki mafunzo hayo walisema awali hawakuwa na uelewa juu ya upangaji wa bajeti lakini sasa wataifanyia kazi elimu waliyopewa.

Pia waliwataka vijana wengine kuwa na nidhamu ya matumizi ya pesa kwa kuweka bajeti pamoja na kuzingatia mahitaji ya lazima.

Jackson Mwakyombe, alisema mafunzo ya upangaji bajeti yamewasaidia kwa kiasi kikubwa vijana kuwa na matumizi sahihi ya fedha wanazozipata kwa kuhakikisha wanaweka vipaumbele.

Mwakyombe alisema elimu ya upangaji bajeti ni muhimu kwa maisha ya kila siku kwani itawawezesha mwananchi kutimiza malengo yao na kuliwezesha taifa kufikia uchumi wa kati.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja Shirika la Elimisha, kupitia wazo lake bunifu la upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia, tayari iwafikia wananchi zaidi ya 8,000 ndani na nje ya mkoa wa Mbeya.



# Dk. Shein awataka watendaji kuwajibika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, ameutaka uongozi na watendaji wa Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kuongeza kasi kipindi hiki kifupi kilichobaki kuelekea uchaguzi mkuu kuwajibika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi.

Alisema hayo jana Ikulu mjini hapa, alipokutana na uongozi wa wizara hiyo wakati ilipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi wa mwaka 2020/2021.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kwa viongozi hao kuongeza kasi katika usimamizi na uwajibikaji wa majukumu ya kazi kwa kuzingatia kuwa shughuli za serikali zinapaswa kuendelezwa kama kawaida hadi pale awamu ijayo ya uongozi itakapochukua nafasi yake. Alisema Zanzibar inahitaji kuwa na uwanja mkubwa wa kisasa utakaowezesha kufanyika shughuli mbalimbali za kitaifa.

Alisema kuna umuhimu wa kuwa na uwanja wa aina hiyo, utakaokuwa na uwezo wa kufanyika matukio mbalimbali ya kitaifa, kama vile gwaride pamoja na michezo ya aina tofauti, ikiwamo mpira wa miguu.

Pia, alisema uwanja uliopo wa Amani hauwezi kukidhi mahitaji ya wakati na kuutaka uongozi wa wizara hiyo kuangalia maeneo ya nje ya mji, likiwamo eneo la Tunguu ambalo limekusanya taasisi mbalimbali na wizara za serikali na kuwa katika mpango huo.

Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Abdulhamid Yahya Mzee, aliwataka watendaji wa wizara hiyo kuwa makini katika usimamizi wa mali na rasilimali za serikali, wakati taifa likielekea kwenye uchaguzi mkuu. Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Ali Abeid Karume, alielezea baadhi ya mafanikio yaliopatikana na wizara hiyo katika kipindi cha miaka mitano ni kutekelezwa kwa Programu ya Ajira kwa vijana, jumla ya vijana 3,490 wamenufaika na programu hiyo.

Alisema wizara hiyo inaendelea na uimarishaji wa kiwanja cha Amani kupitia bajeti yake ya 2019/2020 na shughuli za ujenzi wa mkeka 'base' inaendelea vizuri, huku kazi za uwekaji wa nyasi bandia zikitarajiwa kuanza hivi karibuni.

Wakati huo huo, Dk. Shein, alikutana na uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango na Waziri wa wizara hiyo Balozi Mohamed Ramia, alisema kutokana na athari za ugonjwa wa corona zilizolikabili taifa na dunia, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), tawi la Zanzibar ilikusanya Sh. bilioni 279.70 sawa na asilimia 80 ya matarajio ya kukusanya Sh. bilioni 350.20 kwa mwaka.

Alisema Sh. bilioni 21, ikiwa sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kipindi hicho, yalitokana na chanzo cha kodi ya wafanyakazi wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, katika ofisi za Zanzibar. Alisema serikali imejiwekea mpango maalum wa miaka miwili ili kuhuisha mapato baada ya athari za ugonjwa wa corona, kwa lengo la kuimarisha uchumi wake.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na uongozi wa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, kupitia utekelezaji wa mpango kazi wa wizara hiyo, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, uliofanyika katika ukumbi wa Ikulu mjini Zanzibar, jana. Kulia kwa Rais ni Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Abdulhamid Yahya Mzee na Waziri wa Habari Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo. **PICHA: IKULU**

# Taasisi ya Karume kupokea mil. 300/- kutoka TAE

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAASISI ya Karume ya Sayansi na Teknolojia inatarajia kupokea Sh. milioni 300 kutoka kwa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), ili kuboresha miradi ya elimu Zanzibar.

Mkurugenzi wa TEA, Bahati Geuzye, akizungumza jana katika hafla ya uzinduzi wa jengo la utawala la Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia Zanzibar, alisema kuwa hatua hiyo ni kuendeleza ushirikiano na kuboresha miradi ya elimu Zanzibar.

Alisema katika kufanikisha, tayari Bodi ya Mamlaka hiyo imeidhinisha kiasi hicho cha fedha katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa chuo hicho kwa ajili ya kuendeleza ukarabati wa miundombinu, kuboresha zaidi mazingira ya kujifunza na kufundishia.

Pia, alisema Mamlaka yao imeshiriki katika miradi ya ujenzi na utanuzi wa miundombinu, ununuzi wa vifaa na katika programu mbalimbali za kuboresha upatikanaji wa elimu kwa usawa.

Alisema kati ya mwaka 2012-2016 Mamlaka ya Elimu Tanzania imefadhili programu ya kuwawezesha watoto wa kike kufikia kiwango cha kudahiliwa kuchukua masomo ya sayansi katika elimu ya juu na iliwawezesha watoto wakike 594 kutoka Zanzibar.

Kati ya wanafunzi hao, 345 walisoma katika chuo cha Karume na wengine waliobakia walijiunga na vyuo mbalimbali vya sayansi nchini. Kadhalika TEA itaendelea kushirikiana na taasisi hiyo na nyingine za elimu zilizopo Zanzibar katika kufadhili miradi ya elimu inayolenga kuongeza upatikanaji wa elimu kwa usawa.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idris Muslim Hija, alisema lazima taasisi ya Karume iweke mipango maalumu kwa matengenezo ya dakhalia pamoja na nyumba za taasisi.

Alisema, mpango huo waufanye kwa kupitia Wizara ya Elimu na vyanzo vya mapato vya taasisi wawe wanatenga bajeti ya matengenezo na kutafuta wafadhili wa ndani na nje nchi ili kuyanusuru majengo yasije kuleta maafa.

Ukarabati na ujenzi wa jengo hilo la utawala la chuo hicho limefadhiliwa na TEA ambayo imetoa Sh. milioni 200.

# ZURA kutoa leseni kwa wasambazaji gesi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), inatarajia kutoa leseni kwa wauzaji na wasambazaji wakubwa wa gesi nchini ili kuhakikisha biashara hiyo inaendeshwa kwa misingi ya usalama.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Ofisa Uhusiano wa mamlaka hiyo, Hassan Juma Amour, alisema kuwa hadi sasa mamlaka hiyo imeshapokea maombi ya wafanyabiashara watano wanaoingiza bidhaa hiyo nchini na wasambaji tisa kwa ajili ya kupatiwa leseni.

Alisema, hatua hiyo imefikiwa baada ya mamlaka hiyo kuridhishwa na hatua ya utoaji wa elimu juu ya kanuni ya gesi ya kupikia (LPG) ya mwaka 2017 na miongozo ya gesi kwa ajili ya kusimamia uendeshaji wa biashara hiyo Zanzibar.

Alisema lengo la mamlaka hiyo kutoa leseni hizo ni kuweka usimamizi madhubuti wa biashara hiyo na kujua muingizaji na muuzaji wa rejareja anaendesha vipi biashara hiyo na kama anasimamia misingi ya usalama na viwango vinavyokubalika.

Alisema ZURA imeona umuhimu wa kutoa elimu kabla ya kusimamia sheria na miongozo ili kuhakikisha pale zitakapoanza kutumika ziwe zinafahamika na kufuatwa.

Alieleza kuwa, Zanzibar inategemea soko la Tanzania bara kuagiza nishati hiyo na kampuni zinazofanya biashara hiyo ya jumla ni pamoja na V-Gas, Oryx Gas na Oilcom.

Hassan alisema utoaji wa leseni utawahusisha wauzaji wa rejareja ili kila mtu anakuwa na leseni iliyokuwa kisheria.

Akizungumzia wafanyabiashara wanaouza gesi katika maduka ya vyakula, Hassan alisema kanuni ya gesi inakataza kuchanganya bidhaa hiyo na bidhaa nyingine kwa usalama wa eneo husika.

Kwa upande wake, Kaimu Mkuu wa kitengo cha uhusiano, Khudhaimat Bakar Kheir, alisema ZURA ina jukumu la kusimamia shughuli za nishati ikiwamo gesi ya kupikia majumbani ili isilete madhara kwa watumiaji.

Aliwaomba wafanyabiashara ambao hawajapeleka maombi ya kupatiwa leseni, kuhakikisha wanafanya hivyo ili kuendesha biashara zao kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa na mamlaka hiyo katika kusimamia nishati hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.

## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MBULU (DONGOBESH)**

**TAHANI NIIMA.......................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**DANIEL NIIMA...................................MJIBU MAOMBI**

**Mdaiwa DANIEL NIIMA, popote ulipo.**

Fahamu kwamba mleta Maombi TAHANI NIIMA ameleta Maombi Na.68/2019 dhidi yako.

Hivyo basi kama unakusudia kupinga maombi hayo unatakiwa ulete majibu yako na uwepo Barazani wewe binafsi, wakili wako au mwakilishi anayekubalika kisheria, shauri limepangwa kutajwa tarehe 13.8.2020.

Endapo hautatekeleza hayo shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 18.6.2020.

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MBULU TANZANIA

MWENYEKITI

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MBULU

115856602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;202/2020**

**Ombi la BERNADETA SELESTIN KASSIAN,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu NATALIS HELMAN.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/08/2020.

Tarehe 31.8./2020

Sahihi ya Hakimu

MOROGORO

115856702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA:226..2020**

**Mdai: MARTIN JULIUS NDYALI(WARIDI)**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa: BAKARI RASHIDI**

**Ombi la Mdai: MARTIN JULIUS NDYALI (WARIDI)**

**Kwa: BAKARI RASHIDI**

**Madai ya: PESA SH.950,000/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 18 mwezi 08 mwaka 2020 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 10 mwezi 08 mwaka 2020.

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO.

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

115855902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA:227..2020**

**Mdai: CONGESTA E.KAYENZI (WARIDI)**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa: FATUMA KISWIRI**

**Ombi la Mdai: CONGESTA E.KAYENZI (WARIDI)**

**Kwa: FATUMA KISWIRI**

**Madai ya: PESA SH.5,883,212/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 18 mwezi 08 mwaka 2020 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 10 mwezi 08 mwaka 202

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO.

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

115855802

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI**

**INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB:**

**+255 - 0782253676**

---

## bgtl BEST GROUP (T) LIMITED

Debts collector, Auctioneer, Commission Agent, Broker & Legal Consultant

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **AFRICAN BANKING CORPORATION (T) LTD**, tutauza kwa mnada wa hadhara mali mbalimbali za mdaiwa wao **CHANGJIANG INVESTMENT** ambazo ni sehemu ya dhamana. Mnada utafanyika katika kiwanda cha **MTWARA CEMENT KILICHOPO PEMBA MNAZI eneo la MTWARA MIKINDANI.** Kama inavyoonyesha hapo chini kwenye jedwali;

| NA | JINA LA MDAIWA | AINA YA MALI ZITAKAZOUZWA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | **CHANGJIANG INVESTMENT LIMITED** | MTAMBO WA UJENZI MUUNDO WA XCMG LOADER YENYE USAJILI T.782 CTC, GARI AINA YA TOYOTA KLUGER T 888 CRP, Genereta KVA 68.5, Pikipiki ya tairi 3 yenye na.za usajiri MC 617 BFV, Mota kubwa za kusukuma mitambo, Pamoja na mali nyingine mbalimbali ikiwemo Spea za mitambo ya kutengeneza Cement na Vyuma chakavu. | **29/08/2020** **Kuanzia saa 3:00 Asubuhi** |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mali zitauzwa kama zilivyo
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa. Kwa mali zenye bei ya juu zaidi Tsh.10,000,000/= na mali zitakazouzwa chini ya bei ya 10,000,000/=zitalipiwa malipo yote siku ya Mnada.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku tatu (3). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa Au kuchukua mshindi wa pili.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, au mali na zingine zinazoambatana na hizo ni jukumu la mnunuzi.
5. Baada ya malipo yote mnunuzi atatakiwa kuhamisha mali zake zote, asipo hamisha zitalipiwa storage.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE: +255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Banc ABC**
**Bib titi Mohamed Road,**
**P.O.BOX 31**
**DAR ES SALAAM**
**Tel:+255 222119422**

215856902

---

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

---

## Uza, Chenye Thamani Kubwa

## Kwa Kutangaza Nasi

## Kwa Bei Poa

## Tupigie 0782253676

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuzi kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Serikali yajiuzulu kisa shinikizo la wananchi

**BEIRUT,** Lebanon

WAZIRI Mkuu wa Lebanon, Hassan Diab, alitangaza kujiuzulu kwa serikali yake, kufuatia shinikizo kutoka kwa raia wa nchi hiyo.

Wananchi hao wamekuwa wakishiriki katika maandamano kwa siku kadhaa kufuatia milipuko mikubwa uliotokea mjini Beirut Jumanne wiki jana, iliosababisha maafa na hasara kubwa.

Milipuko hiyo ilisababisha vifo vya takriban watu 160 na zaidi ya 5,000 kujeruhiwa.

Waandamanaji hao wamekuwa pia wakitaka serikali ya Diab kujiuzulu, kwa shutuma za uongozi mbaya na kuhujumu uchumi wa nchi hiyo.

Katika hotuba iliyorushwa moja kwa moja na vituo vya televisheni nchini humo, Diab alisema amechukua hatua hiyo ili kutoa nafasi ya kuokoa Lebanon, na kuongeza kwamba raia wa nchi hiyo watashiriki katika mchakato huo.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Diab alisema kuwa "Mungu isaidie Lebanon".

Diab aliunda serikali Januari mwaka huu, baada ya kutokea kwa vuta ni kuvute ya kisiasa, ambayo hata kabla ya hapo, mara kwa mara ilikuwa ikishuhudiwa nchini humo.

Kabla ya tangazo la kujiuzulu kwa utawala wake Jumatatu, mawaziri na wabunge kadhaa tayari walikuwa wamejiuzulu.

Milipuko ya Jumanne, ambayo inadaiwa kusababishwa na kemikali aina ya Ammonium Nitrate, inakadiriwa kusababisha hasara ya takriban dola bilioni tano za Marekani. **VOA**

# Waliofariki kwa corona Kenya wafikia 438

**NAIROBI,** Kenya

IDADI ya watu waliopoteza maisha nchini Kenya kutokana na janga la ugonjwa wa corona imefikia 438, baada ya watu wengine 15 kufariki duniani katika kipindi cha saa 24 zilizopita.

Aidha, idadi ya watu walioambukizwa imeongezeka na kufikia zaidi ya 27,400 baada ya watu wengine 497 kuripotiwa kuambukizwa.

**Idadi ya watu walioambukizwa imeongezeka na kufikia zaidi ya 27,400.**

Waziri wa Afya nchini humo, Mutahi Kagwe, aliwataka wananchi wa Kenya kuendelea kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa corona katika maambukizi.

Wakati nchi hiyo ikiendelea kukabiliana na janga hilo, Wizara ya Afya imeendelea kupata shinikizo za kuweka wazi kuhusu namna inavyotumia fedha za kukabiliana na janga hilo.

Virusi vya ugonjwa wa corona vilibainika kwa mara ya kwanza katika mji wa Wuhan katikati mwa China, mwishoni mwa Desemba mwaka jana, na vimehusishwa na soko la jumla la vyakula, ambako wanyama wa porini wanauzwa.

Hivi karibuni, Shirika la Afya Duniani (WHO), lilionya kuwa licha ya jitihada zinazofanyika kutafuta chanjo na dawa ya kupambana na janga la virusi vya corona, huenda kusiwe na suluhu ya muda mrefu ya kukabiliana na janga hili. **VOA**




Seneta Kamala Harris (Kulia) na Makamu wa Rais wa zamani, Joe Biden (Kushoto). **PICHA: REUTERS**

# Biden amteua seneta Harris mgombea mwenza

**WASHINGTON DC,** Marekani

MGOMBEA urais wa Marekani kwa tiketi ya Chama Cha Democratic, Joe Biden, alimteua Seneta wa jimbo la California, Kamala Harris, kama mgombea mwenza katika uchaguzi wa urais unaotarajia kufanyika Novemba, mwaka huu.

Kwa kumteua Harris, Biden aliweka historia kwani ni mara ya kwanza kwa mwanamke mweusi kuwa kwenye tiketi ya kuwania urais kupitia chama kikubwa cha kisiasa cha Marekani.

Aidha ni ishara ya Biden kukiri kwamba wapiga kura weusi watakuwa na nafasi kubwa katika azma yake ya kumshinda Rais Donald Trump anayewania muhula wa pili kwa tiketi ya chama cha Republican.

Seneta Harris, mwenye umri wa miaka 55, ni mmoja wa watu mashuhuri sana ndani ya chama hicho, na alitajwa kama mmoja wa watu ambao wangeteuliwa kuwa wagombea-wenza wa Biden punde tu alipositisha kampeni yake ya kuwania uteuzi wa chama.

Anaungana na Biden kwenye kampeni wakati ambapo kuna mzozo wa kitaifa ambao haujawahi kushuhudiwa.

Mlipuko wa virusi vya corona umesababisha vifo vya watu zaidi ya 150,000 nchini Marekani, ambayo ni idadi kubwa zaidi kuliko ilivyo katika nchi nyingine kote duniani.

Biashara zimefungwa huku janga hilo likisababisha kudorora kwa uchumi. Wakati huo huo, maandamano na ghasia zimeshuhudiwa katika miji mbalimbali, Wamarekani wakilalamikia ubaguzi na ukatili wa maofisa wa polisi.

Hakuna mwanamke ambaye amewahi kuwa Rais au Makamu wa Rais nchini Marekani. Ni wanawake wawili tu ambao wamewahi kuteuliwa na vyama vikuu vya Marekani kuwa wagombea wenza katika historia ya Marekani.

Geraldine Ferraro kutoka chama cha Democratic mwaka 1984 na Sarah Palin, wa chama cha Republican, aliyeteuliwa na Marehemu John McCain mwaka 2008. Hata hivyo, hawakufanikiwa kushinda.

Rais Donald Trump anaelekea kwenye uchaguzi akiwa na makamu wake, Mike Pence, kama mgombea mwenza. **VOA**

## Wasio wanasiasa kuunda baraza la mawaziri

**TUNIS,** Tunisia

WAZIRI Mkuu mteule nchini Tunisia, Hicehm Mechichi amesema kwamba ataunda Baraza la Mawaziri lenye watu ambao sio wanasiasa, kufuatia mzozo usiomalizika kati ya vyama vya kisiasa kuhusu uundwaji wa serikali mpya.

Hatua ya Hicehm Mechichi, huenda ikamuweka katika hali ya mvutano na chama cha Ennahda chenye wabunge wengi, ambacho tayari kimesema kwamba kitapinga kabisa hatua yoyote ya kuteua serikalini watu ambao sio wanasiasa.

Hata hivyo, pendekezo la kuunda serikali ya wataalam wasioegemea kundi lolote la kisiasa, huenda likapata uungwaji mkono mkubwa kutoka kwa muungano wa wafanyakazi wenye nguvu sana nchini Tunisia -UGTT, Pamoja na vyama vingine vya kisiasa, vikiwemo Tahya Tounes na Dustoury el Hor.

Mechichi alisema kwamba lengo la serikali litakuwa kutatua hali ngumu ya maisha wanaopitia watu wa kawaida na kujenga uchumi ambao umeharibika.

Hata hivyo, alikashifu wanasiasa kwa kuzozana wakati raia wa kawaida hata hawana maji safi ya kunywa.

Maandamano yametokea katikati mwa Tunisia mwaka huu kulalamikia ukosefu wa ajira na huduma mbovu serikalini hasa za afya, ukosefu wa maji na umeme. **VOA**



# LOPETEGUI: SEVILLA ITAWAZIMA UNITED

**DUISBURG,** Ujerumani

JULEN Lopetegui amesema Manchester United ni "timu kubwa sana duniani "lakini anajiamini Sevilla watawasimamisha Jumapili kwenye nusu fainali ya Kombe la Ligi ya Europa.

Miamba hao wa LaLiga wametinga hatua hiyo na sasa watawavaa mabingwa hao wa mwaka 2017, United mjini Cologne baada ya ushindi wao wa 1-0 dhidi ya Wolves, Jumatano.

Mapema Yassine Bounou aliokoa penalti ya Raul Jimenez na kuanzia hapo Sevilla ikaongeza mashambulizi hadi walipopata bao hilo kupitia kwa Lucas Ocampos zikiwa zimesalia dakika mbili mpira kumalizika.

United iliifunga Copenhagen bao 1-0 katika muda wa ziada Jumanne na sasa kikosi hicho cha Lopetegui kitavaana na 'Mashetani Wekundu' hao.

"Tunakwenda kucheza dhidi ya Manchester United mchezo wetu unaofuata- wao ni timu kubwa sana duniani, lakini tutajianda kwa ajili yao," alisema Lopetegui akiwaambia waandishi wa habari.

"Tumejipanga kwa ajili ya mchezo ujao, dhidi ya timu yenye historia, moja ya timu bora kwenye historia ya mchezo huu.

"Tutacheza kwa kiwango chetu bora kabisa. Kucheza dhidi yao kwa hakika utakuwa mchezo mgumu kwetu, lakini tunakwenda huku tukiamini tunaweza kuwasimamisha."

# Wakala akanusha Pirlo kumkataa Ramsey Juventus

**TURIN,** Italia

WAWAKILISHI wa kiungo wa Juventus, Aaron Ramsey wamekanusha uvumi kwamba kocha mpya wa kikosi hicho, Andrea Pirlo yupo tayari kumuuza.

Pirlo aliteuliwa kocha mkuu wa Juve, akiwa ametumia kama wiki moja tu kuwa kocha wa kikosi cha Juve chini ya umri wa miaka 23, baada ya Maurizio Sarri kufukuzwa kutokana na kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa hatua ya 16-bora mikononi mwa Lyon.

Ripoti ya gazeti la Mirror ilidai Pirlo hamuoni Ramsey kama sehemu ya mipango yake na anaonana mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 raia wa Wales kuangalia uwezekano wa kutafuta klabu mpya.

Hata hivyo, Avid Sports & Entertainment Group, kampuni ambayo inamuwakilisha Ramsey imeeleza kwamba uvumi huo ni "upuuzi" kupitia kwenye Twitter.

Ramsey amekumbwa na wakati mgumu katika msimu wake wa kwanza kule Juve baada ya kujiunga nao Julai, mwaka jana, akitoka kucheza kwa miaka 11 kule Arsenal.

Ingawa ameshinda taji la Ligi Kuu ya Italia, Scudetto, alianza katika mechi 11 tu za Ligi wakati Sarri alipokuwa anashindwa kumtafutia nafasi ya kudumu kwenye kikosi chake.

Ramsey, ambaye analipwa mshahara wa euro 400,000 kwa wiki pale Turin, amekuwa akihusishwa na uwezekano wa kutua Manchester United.





# *Wolves inahitaji nyota zaidi- Nuno*

**DUISBURG,** Ujerumani

WOLVES inahitajii kusajili wachezaji zaidi ili kukifanya kikosi chake kuwa imara, amesema kocha, Nuno Espirito Santo baada ya kutolewa kwenye robo fainali ya Ligi ya Europa na Sevilla.

Msimu wao ulihitimishwa kwa siku 383 na mechi 59, na hawatashikiri michuano hiyo msimu ujao baada ya kumaliza nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England.

"Tunahitaji wachezaji zaidi kutusaidia sisi, ni kikosi kidogo," alisema Nuno. Wolves walitolewa kwa bao la kichwa la Lucas Ocampos dakika za majeruhi, baada ya awali Raul Jimenez penalti yake kuokolewa.

Walitumia wachezaji 21 tu kwenye ligi msimu huu, ikiwa ni pungufu ya watatu kuliko kikosi chochote.

Juu ya hilo kwenye Ligi ya Europa walikuwa na wachezaji 17, na nane kati yao walicheza jumla ya 50 au zaidi. Nuno alisema: "Ni muda wa kujipanga. Tunahitaji kupumzika, mapumziko makubwa. Tunatakiwa kujiandaa vizuri kwa ajili ya msimu ujao na kufanya uamuzi mzuri utakaoturuhusu kuendelea kukua.

"Ni muda wa kuangalia nyuma na kufanya uchambuzi kwa kina. Timu iliyoanza kwenye mchezo huu ni ile ile iliyoanza mchezo wa kwanza wa msimu. Tumefanya makosa hatuwezi kuyarudia."

# Lindelof: Kombe la Europa linatuhusu

**MANCHESTER,** England

VICTOR Lindelof amesema Manchester United iliwatoa FC Copenhagen, lakini amesisitiza bado wana nafasi ya kutosha kushinda taji la Ligi ya Europa.

Kikosi hicho cha Ole Gunnar Solskjaer kilihitaji bao la penalti la dakika za majeruhi kutoka kwa Bruno Fernandes kuwaondoa Copenhagen mjini Cologne, Jumatatu usiku na kutinga nusu fainali.

Na sasa United itacheza na Sevilla kwenye nusu fainali ya mashindano hayo Jumapili na Lindelof amesema wanatakiwa kuwa bora ili kupata nafasi ya kufuzu kucheza fainali kule kwenye dimba la RheinEnergieSTADION, Agosti 21.

"Inatokea muda mwingine kwenye soka," alisema.

"Bila shaka umekuwa ni msimu mrefu, lakini tumecheza robo fainali ya Ulaya na nafikiri kila mmoja anatakiwa kuwa tayari kwa nusu fainali.

"Kama nilivyosema, huwa inatokea kwenye soka kwamba huchezi katika kiwango unachokitaka. Lakini kitu cha muhimu ni kwamba tumeshinda na tumetinga nusu fainali."






# PIERRE-EMILE ATUA RASMI SPURS

**LONDON,** England

TOTTENHAM Hotspur imekamilisha usajili wa Pierre-Emile Hojbjerg kutoka Southampton.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Denmark amesajili mkataba wa miaka mitano baada ya kufuzu vipimo vya afya Jumatatu na kuwa usajili wa kwanza wa kocha, Jose Mourinho kipindi hiki cha majira ya joto, akijiunga kwa ada ya pauni milioni 15.

Katika dili hilo mlinzi wa kushoto, Kyle Walker-Peters mwenye umri wa miaka 23, ameondoka Spurs na kujiunga Southampton kwa mkataba wa miaka mitano baada ya kucheza kwa mkopo klabuni hapo nusu ya msimu uliopita. Hojbjerg amecheza mechi 134 kwa Southampton baada ya kujiunga nayo akitokea Bayern Munich mwaka 2016, na akawa nahodha wa 'watakatifu' hao kabla ya kupokonywa unahodha Juni wakati alipothibitisha anataka kuondoka klabuni hapo.

"Kitu muhimu nilichokuwa nakitaka mimi ni kujiona mwenyewe nikicheza katika klabu ambayo naona naweza kucheza kwa miaka mingi, na Tottenham ni moja wapo," alisema Hojbjerg akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Najisikia fahari kubwa, nina furaha na nimehamasika kwelikweli. Nafikiri sehemu bora kwangu kwa siku zijazo na nataka kuwa sehemu ya klabu hii kwa muda mrefu. "Spurs ina wachezaji wanaovutia, kocha mzuri na mazingira yake pia ni mazuri sana.

"Najisikia bahati na fahari kuwa sehemu ya klabu hii, nitajitoa kwa hali na mali kuhakikisha naisaida klabu, huku nikicheza kwa kiwango changu bora kabisa."

# *AC Milan yawania kumsajili Bakayoko*

**MILAN,** Italia

AC Milan ipo kwenye mazungumzo juu ya kumrudisha kiungo wa Chelsea, Tiemoue Bakayoko hapo San Siro, kwa mujibu wa Sky in Italia.

Milan wanataka kumsajili Mfaransa huyo katika dili la awali la mkopo wa euro milioni tatu na kutakuwa na kipengele cha kumsajili moja kwa moja kwa euro milioni 35.

Bakayoko atakutana na mazingira aliyoyazoea kama atatua kule Milan, awali akiwa amecheza hapo mechi 42 wakati akiwa kwa mkopo msimu wa 2018/19.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ameshindwa kupenya kwenye kikosi cha kwanza pale Chelsea tangu alipotua akitokea Monaco kwa ada ya pauni milioni 40 mwaka 2017, na alitumia msimu uliopita akicheza kwa mkopo kwa miamba hao wa Ligue 1.

Sky Sports iliripoti mapema mwezi huu kwamba, Bakayoko ni mmoja wa wachezaji ambao Chelsea ipo tayari kuwauza kwa ajili ya kutafuta fedha ili iingie kwenye soko la usajili.

Frank Lampard tayari ameongeza Hakim Ziyech na Timo Werner kwenye kikosi chake.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DEMBELE MBADALA WA SANCHO UNITED

●●● Sasa wanafikiria kubadili gia angani kwani wanataka kuanza mazungumzo...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United itaendelea kushawishi dili la winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho lakini sasa wanamkodolea macho nyota wa Barcelona, Ousmane Dembele kama mbadala wake, kwa mujibu wa nyanzo vya ESPN.

**Mkurugenzi wa Dortmund, Michael Zorc aliondoa uwezekano wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, kuhamia Old Trafford wakati aliposema klabu "inapanga kuwa na Sancho kwenye timu yetu msimu huu," akiongeza kwamba maamuzi juu ya majaliwa yake ni ya "mwisho."**

Ingawa Sancho anataka kujiunga na United huku maslahi binafsi ikiwa si kitu kinachotarajiwa kuwa tatizo, Dortmund wanaendelea kushikilia msimamo wao wa kutaka euro milioni 120 ili kumuachia mchezaji huyo.

United wanaamini kwamba kiasi hicho cha fedha ni kikubwa mno hasa kutokana na uchumi kuathirika na mlipuko wa virusi vya corona.

Zorc pia amebainisha kwamba mkataba wa Sancho uliongezwa kipindi cha majira ya joto kilichopita kwa mwaka mmoja zaidi na kwamba atabaki klabuni hapo hadi mwaka 2023.

Sancho alijiunga na wachezaji wenzake wa Dortmund Jumatatu kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya ambapo wameweka kambi nchini Uswisi na miamba hao wa Bundesliga waliweka Agosti 10 ndio siku ya mwisho ya United kufikia makubaliano.

Hata hivyo, United sasa wanafikiria kubadili gia angani kwani wanataka kuanza mazungumzo na Dembele ambaye pia ni mchezaji wa zamani wa Dortmund.

Vyanzo hivyo vimeipasha ESPN kwamba, United imeanzisha mazungumzo juu ya uwezekano wa kumsajili Dembele, ambaye amebakiza miaka miwili katika mkataba wake kule Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, hajacheza mechi ya kimashindano tangu Novemba mwaka jana na alifanyiwa upasuaji Februari mwaka huu.

Miaka yake mitatu na miamba hao wa Catalunya imekuwa migumu kwake kwa kukumbwa na majeruhi ya mara kwa mara, na sasa Dembele anaweza kuhitaji kuishawishi Barcelona kuondoka, huku Man United wakimtolea macho kwa karibu.

## ZISIKUPITE

### SILVA HUYO LAZIO

KIUNGO wa Manchester City, David Silva mwenye umri wa miaka 34, atajiunga na Lazio wakati mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Guardian)***

### CHAMBERS AWINDWA FULHAMU

FULHAM inafikiria kumsajili mlinzi wa Arsenal, Calum Chambers mwenye umri wa miaka 25, huku Muingereza huyo akitarajiwa kuwagharimu pauni milioni 12. ***(Sun)***

### BAYERN KUMUACHIA THIAGO

AFISA Mtendaji Mkuu wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge, yupo tayari kuzungumza na klabu itakayohitaji kutoa ofa ya maana kwa kiungo, Thiago Alcantara mwenye umri wa miaka 29, ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool. ***(Mail)***

### IMMOBILE AMULIKWA N'CASTLE

STRAIKA wa Lazio, Ciro Immobile amedai Newcastle imewasiliana na wakala wake juu ya uwezekano wa kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto - lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, anataka kubaki na klabu hiyo ya Serie A. ***(Corriere dello Sport - via Goal)***

### ASTON VILLA KWA WATKINS

ASTON Villa wanaandaa ofa kwa straika wa Brentford, Muingereza Ollie Watkins mwenye umri wa miaka 24. ***(Sky Sports)***

### BALE BADO YUPO REAL

GARETH Bale hataondoka Real Madrid kipindi hiki cha majira ya joto - na mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales mwenye umri wa miaka 31, anajiandaa kusubiri kwa miaka miwili kabla ya kutafuta klabu mpya. ***(Mirror)***

### ARSENAL WAMTAKA PROMES

KLABU ya Arsenal inangalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Ajax wa Uholanzi, Quincy Promes mwenye umri wa miaka 28 kwa pauni milioni 25. ***(Sun)***

### CHELSEA KUMUUZA PALMIERI

CHELSEA ipo tayari kumuuza mlinzi wake wa kimataifa wa Italia, Emerson Palmieri, huku Inter Milan ikiwa ipo tayari kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Football Insider)***

### CEBALLOS KUBAKI MADRID

REAL Madrid inataka kumbakiza kiungo wa kimataifa wa Hispania, Dani Ceballos mwenye umri wa miaka 24, klabuni hapo baada kurudi kutoka kucheza kwa mkopo wa muda mrefu kule Arsenal. ***(AS)***

### LEICESTER KUMSAJILI MCNEIL

KLABU ya Leicester City imeonyesha nia ya kutaka kumsajili winga wa Burnley, Dwight McNeil mwenye umri wa miaka 20, raia wa Uingereza. ***(Sky Sports)***

### FRASER AGOMBEWA EPL

KLABU zilizopanda Ligi Kuu, West Bromwich Albion, Leeds na Fulham zipo kwenye mbio moja kuwania kumsajili winga wa kimataifa wa Scotland, Ryan Fraser mwenye umri wa miaka 26, ambaye aliondoka Bournemouth mwishoni mwa Juni akiwa huru baada ya kumaliza mkataba wake. ***(90Min)***

## Twiga yaibwaga Simba Kings

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Kriketi ya Twiga Titans imeonyesha nia ya kuwa moja ya klabu zinazopewa nafasi ya kufanya vizuri katika ligi ya mchezo huo iitwayo APL baada ya kuibuka na ushindi wa wiketi tano iliyoupata dhidi ya Simba Kings katika mechi iliyofanyika katika viwaja vya Klabu ya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana.

Ulikuwa ni ushindi wa tatu kwa klabu hiyo katika ligi hiyo, iliyoanza wikiendi iliyopita ikitarajiwa kuhitimishwa mwishoni mwa wiki hii.

Katika mechi ya jana, Simba Kings walipata fursa ya kuanza kupiga mpira wakapata mikimbio 109 huku wakipoteza wiketi sita katika ova 20.

Kapteni wa klabu hiyo, Zafar Khan aliingia uwanjani kuisaidia timu kupata mikimbio akitokea benchi na kuisaidi kwa kufunga mikimbio 43 na kuwa mchezaji aliyefunga mikimbio mengi zaidi katika timu hiyo.

Wachezaji wengine, Stewart Kaduma na Muzamil Hussain, pia walijitahidi kuonyesha mchezo mzuri ambapo Kaduma alipata mikimbio 19, Hussain akipata mikimbio 14.

Twiga Titans ambayo ilifanikiwa kufikisha idadi ya mikimbio iliyotakiwa ili ipate ushindi, ambayo ni 110, huku ikipoteza wiketi tano katika ova 18.1, inatarajiwa kurudi uwanjani leo kuchuana na Chui Challengers katika mechi ya kwanza ya siku, itakayochezwa asubuhi ikifuatiwa na Buffalo Blasters dhidi ya Tembo Stars.

## JKU, KVZ kuvaana nusu fainali FA Cup

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU za JKU, KVZ na Dulla Boys zimetinga hatua ya nusu fainali ya Kombe la ZFF (FA Cup) linaloendelea Kisiwani Unguja huku Kisiwani Pemba likifikia hatua ya robo fainali.

JKU ambayo ipo Ligi Kuu Zanzibar, imetinga hatua hiyo kwa mikwaju ya penati 4-2 dhidi ya timu ya Gulioni FC iliyopo Ligi Daraja la Pili Mkoa wa Mjini Magharibi baada dakika 90 kumalizika kwa kutoshana nguvu.

Akizungumza na gazeti hili Katibu wa JKU, Sadu Ujudi, alisema malengo yake makubwa ni kuhakikisha anafanya vizuri katika michuano hiyo na kupata nafasi ya kuiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika (Caf).

Alisema baada ya kupenya katika hatua ya robo fainali, sasa wanajipanga kucheza nusu fainali dhidi ya KVZ, katika mechi ambayo anaamini itakuwa ngumu kutokana upinzani mkali zinapokutana kwenye Ligi Kuu.

"Tumeingia nusu fainali, na matarajio yetu tuhakikishe tunatinga hatua ya fainali na hata kupata nafasi ya kushiriki Kombe la Shirikisho Afrika, tumekosa ubingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar matumaini yetu tumewekeza Kombe la shirikisho," alisema.

# SENZO AMPONZA MBAGA SIMBA, MANARA AKALIA KITI

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umemsimamisha kazi Mkurugezi wa Wanachama na Mashabiki wa klabu hiyo, Hashim Mbaga, huku nafasi yake kwa sasa ikikaimiwa na Ofisa Habari wa miamba hiyo, Hajji Manara.

**Taarifa zilizolifikia gazeti hili kutoka chanzo chetu ndani ya klabu hiyo, zimedai kuwa uongozi umechukua uamuzi wa kumsimamisha Mbaga kwa sababu ya kutokuwa na imani naye.**

Kimeeleza kuwa hatua hiyo ni baada ya kuhofia kiongozi huyo kuwa na ukaribu mkubwa na aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingiza aliyejiuzulu nafasi hiyo hivi karibuni na kuhamia Yanga.

"Mbaga yupo karibu sana na Senzo aliyehamia Yanga, hivyo kuondoka kwa mtendaji huyo kumewafanya viongozi wasiwe na imani naye, hivyo wamechukuwa uamuzi wa kumuondoa katika nafasi hiyo.

"Suala kubwa la kumuondoa ni kuhofia mambo yao kuvuja, hivyo nafasi yake kwa sasa kukaimiwa na Manara ambaye ameonekana viatu vya nafasi hiyo kumtosha ," kilieleza chanzo chetu.

Alipotafutwa Katibu Mkuu wa Simba, Arnold Kashembe, alisema hawezi kulitolea kauli jambo hilo huku akiwataka mashabiki na wanachama kuwa na imani na uongozi wao.

Alisema taarifa hizo zitatolewa rasmi na kitengo chao cha habari, na kwamba anaamini ndani ya Simba hakuna mtu mkubwa kuliko klabu hiyo na atakayetoka ndani ya uongozi viongozi hufanya mchakato wa kupata mtu mwenye weledi zaidi.

"Mashabiki na wanachama wetu watulie na wanatakiwa kuwa na imani na viongozi, Simba ni taasisi kubwa anapotoka mtu anakuja mtu zaidi ya aliyeondoka, wanatakiwa kutulia kwa sababu tunafanya kazi kisasa zaidi," alisema Kashembe.

Alisema kuna mambo mazuri yanakuja Simba ikiwamo usajili wa wachezaji wao wapya ambao watakuja kuongeza nguvu ndani ya kikosi cha timu hiyo kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Katika usajili mambo yanaenda vizuri, tumesajili kulingana na mahitaji ya benchi la ufundi linaloongozwa na Sven Vandenbroeck, ambaye tunatarajia atarejea Agosti 17, mwaka huu," alisema Katibu huyo.

Simba inatarajia kuingia kambini Agosti 17 kuanza maandalizi ya "Simba Day" inayotarajiwa kufanyika Agosti 22, mwaka huu ikiwa ni pamoja na kujiandaa na mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Namungo FC na Ligi Kuu Bara.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko, Mawasiliano na Mahusiano wa KCB, Christina Manyenye (kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 10 kwa ajili ya Mfungaji Bora wa Ligi Kuu Bara msimu wa 2019/20. Anayepokea ni Meneja wa timu ya Simba, Patrick Rweyemamu, kwa niaba ya Meddie Kagere aliyeibuka kinara kwa kufunga mabao 22, katika sherehe za utoaji wa tuzo hizo zilizofanyika Ijumaa iliyopita. **NA MPIGAPICHA WETU**

# KCB yajivunia kuichangamsha Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

BENKI ya KCB, imesema kwa kipindi cha miaka miwili ikiwa miongoni mwa wadhamini wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imeichangamsha ligi hiyo kwa kuifanya kuwa bora na ya kuvutia, huku ikigundua kwamba soka ni ajira na limewasaidia vijana wengi kujikwamua na umasikini.

Aidha, imeeleza kufurahi kuona vipaji vingi vya vijana vikiibuliwa kwenye soka hasa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu hii miwili, ambayo nao ni miongoni mwa waliotoa mchango huo.

Akizungumza na Waandishi wa Habari juzi, Mkuu wa Kitengo cha Masoko, Mawasiliano na Uhusiano, Christina Manyenye, alisema kwa vipindi viwili mfululizo yaani msimu wa 2018/19 na 2019/20 wakiwa sehemu ya wadhamini wa Ligi Kuu Tanzania Bara, walishirikiana vema na Shirikisho la Soka nchini (TFF), katika mkakati wa kukuza soka nchini kwa vijana.

Alisema hatua hiyo imewasaidia vijana kuondoa umasikini kwenye jamii, lakini pia inachangia maendeleo kwa kuinua na kukuza vipaji vya vijana wengi, hivyo wao wanajiona hawajafanya kosa kabisa kujiingiza kwenye udhamini kusaidia Ligi Kuu.

"Mchango wetu kwa kiasi kikubwa kwa sasa upo kwenye kuboresha mpira wa mguu nchini kwa kushirikiana na benki yetu ya KCB, mbali na hilo tumekuwa tukitoa mchango katika kudhamini mpira wa miguu Tanzania katika ligi mbalimbali ndani na nje ya nchi, na kwa kuongezea tulikuwa pia miongoni mwa wadhamini wa Kombe la FA mwaka 2018 kwenye mechi ya fainali ya Arusha mwaka jana iliyofanyika mkoani Lindi na hii ya hivi majuzi kati ya Simba na Namungo, iliyofanyika Sumbawanga," alisema Ofisa huyo.

Alisema juhudi zao kwa sasa zinajikita kusaidia vijana kuwa wafanyabiashara, wanamichezo au wajasiriamali ili kujitegemea kiuchumi wanapomaliza masomo, huku wakidhamini baadhi ya vijana kwenye Chuo cha Mafunzo Stadi (VETA).

Michezo
Alhamisi Agosti 13, 2020
Nipashe



Dembele mbadala wa Sancho United

UKURASA 22

KIMEELEWEKA...



Mashabiki wa soka walivyopokea hukumu ya kiungo wa Yanga, Bernard Morrison, dhidi ya klabu yake, nje ya ofisi za Shirikisho la Soka nchini (TFF) Karume jijini Dar es Salaam, baada ya mchezaji huyo kutangazwa kushinda jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NI MO MO MO MORRISOOON!

## ●●● Sababu kuibwaga Yanga TFF, atakiwa kurejesha mamilioni Jangwani...

**Na Saada Akida**

MO mo mo Morrison karibu Simba! Hivyo ndivyo kelele zilivyolipuka nje ya geti la Ofisi za Shirikisho la Soka nchini (TFF) zikitoka kwa mashabiki wa Simba kabla na baada ya kiungo wa Yanga, Mghana Bernard Morrison jana kushinda shauri lake dhidi ya klabu yake hiyo kuhusu mkanganyiko wa mkataba wake mpya.

**Shauri lililokuwa likisikilizwa lilitokana na Morrison kudai mkataba wake ni wa miezi sita na umekwisha muda wake huku Yanga ikieleza kuwa alisaini dili lingine la miaka miwili, lakini mchezaji huyo akieleza hautambui huo mwingine na saini yake ilighushiwa.**

Lakini baada ya kesi hiyo kusikilizwa na Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF kwa muda wa siku tatu mfululizo kuanzia Agosti 11 huku ikivuta hisia za mashabiki na wadau wengi wa soka ndani na nje ya nchi, jana jioni hukumu hiyo ikatoka na Morrison kuibwaga Yanga.

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF, Elias Mwanjala, akitoa sababu za mchezaji huyo kushinda alisema mkataba wa Yanga na Morrison, una upungufu mkubwa upande wa Yanga, hivyo wamempa faida Morrison.

"Tumekuwa makini katika kufuata haki na kamati yetu ilikuwa makini, kulikuwa na upungufu mkubwa upande wa tarehe ambapo kuna sehemu ilionyesha kuwa amesaini Machi 20 huku chini ukionyesha Julai 15, 2020.

"Pia kuna ukurasa wa saini kwenye mkataba unaonyesha kuna upungufu katika sehemu ya saini ambayo imefutwa kwa kalamu jambo ambalo linaonyesha kwamba kulikuwa kuna tatizo kwenye masuala ya mkataba, ni upungufu mkubwa, hivyo tunampa ushindi Morrison anakuwa mchezaji huru, suala la timu atakayocheza itakuwa ni uamuzi wake," alisema Mwanjala.

Mwanjala aliongeza: "Kazi yetu tumemaliza ila Morrison anapelekwa Kamati ya Maadili ya TFF kutokana na kosa la kusaini mkataba na timu nyingine (Simba), wakati kesi yake inaendelea kusikilizwa.

"Kesi inayokwenda Kamati ya Maadili, haina uhusiano na hii ya Yanga dhidi ya Morrison, ambayo yeye ameshinda na ni mchezaji huru. Mchezaji mwenyewe amekiri kuwa amefanya hivyo, ikiwa Yanga hawajaridhika na uamuzi huu ni ruksa kwenda kukata rufaa."

Aidha, mwenyekiti huyo alisema Morrison amekiri katika kamati hiyo kwamba alichukua kiasi cha dola 30,000 (sawa na Sh. 69,528,900 za Tanzania) kutoka kwa Yanga ambazo ameahidi kuzirudisha kwa uongozi wa timu hiyo.

Alisema endapo Yanga hawajaridhika wanatakiwa kupitia upya hukumu hiyo au kuiandikia barua kamati ama kufikisha suala hilo kwa Mahakama ya Usuluhishi ya mambo ya Soka ya Kimataifa (CAS).

# Wasiojulikana watibua Sure Boy kutua Yanga SC

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya awali, Azam FC kuisifu Yanga kwa kufuata taratibu stahiki kwenye mpango wao wa kuipata huduma ya kiungo Salum Abubakary 'Sure Boy', mchakato huo sasa umegeuka wa kutaka kuombana radhi kila upande huku 'wasiojulikana' wakihusishwa katika kuufanikisha, imefahamika.

Juzi usiku Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Azam, Thabiti Zakaria 'Zaka Zakazi', alinukuliwa akieleza kuwa licha awali Yanga kufuata taratibu, lakini baadaye waligeuka na kuzungumza na mchezaji wao kinyume cha taratibu jambo ambalo aliitaka klabu hiyo kuomba radhi.

Zakazi alisema: "Awali Yanga walileta barua ya kuonyesha nia ya kumsajili tukakataa, lakini baadaye tulipomuweka Sure Boy sokoni wakaja na ofa ya Sh. milioni 20, tukakataa, baadaye wakaja na Sh. milioni 35 tukakataa, na mtu aliyekuwa akitumwa kuleta ofa hizo ndiye huyo huyo aliyeleta barua ikionyesha imetoka kwa Sure Boy.

"Barua yenyenye tumeipata Agosti 11, lakini inaonyesha ilitakiwa kuja kwetu Agosti 12, na tulipomuuliza mchezaji wetu alikataa kuwa si yeye aliyeandika, hivyo inaonyesha Yanga walikuwa wanazungumza na mchezaji wetu kinyume cha taratibu wakati bado ana mkataba wa mwaka mmoja."

Lakini jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alikuja juu kwa kueleza amesikia madai hayo yaliyotolewa na Zakazi, lakini Klabu ya Yanga haijatuma mtu yeyote kupeleka barua hiyo na kuitaka Azam FC kama wanamfahamu wamtaje ili waweze kumchukulia hatua.

"Tatizo wao wanatafuta followers (wafuasi) na kuwa front page (ukurasa wa mbele) wa magazeti, sisi hata kama tusiposajili utakuta kesho tupo ukurasa wa mbele, wanatafuta 'kiki' kama kuna mtu kapeleka hiyo barua waje mbele wamtaje vinginevyo tutapelekana mbele.

"Kuna watu wanachafua brand (chapa) ya Yanga, wamtaje huyo mtu tumjue alipeleka hiyo barua kwa interest (maslahi) gani, maana sisi hatumjui, watu wetu wote wana ID (kitambulisho), tunataka tumjue ID yake ni namba ngapi," alisema Bumbuli.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >